# Pambazuko

Toleo Namba 170 | Jumatatu, Juni 22-28, 2026


# Oktoba 29 bado yauma

- Miundombinu iliyoharibiwa yasuasua ukarabati

Uk. 6&7



*Kituo cha Mabasi Yaendayo Haraka (Udart) cha Magomeni bado hakijaanza kukarabatiwa baada ya kuharibiwa kwenye vurugu za Oktoba 29, 2025. Kamera ya Pambazuko ilipiga picha hii jana.*

## Wanaopotosha elimu ya lishe mitandaoni kukiona

**KATIKA kipindi hiki cha dunia ya kidijitali, mitandao ya kijamii imekuwa jukwaa kuu la kusambaza taarifa...**

Habari Uk. 20

**Tafakuri ya Bagonza**

## Tuna msiba usiokuwa na mwili wa marehemu

Safu Uk. 10

## Madhara uamuzi Bunge la Ulaya kwa Tanzania Uk. 15

# Bajeti ya kujenga uchumi kidigitali



**Sasa ni mwendo wa kidigitali kuanzia miamala ya ardhi, magari hadi nauli za usafiri na biashara ndogo, serikali inaamini teknolojia ndiyo ufunguo wa uwazi wa kiuchumi, ujumuishaji wa kifedha na kujitegemea** Uk. 12




**Jicho la Tai**

## Baba siyo jina pekee, ni wajibu uliotukuka

Safu Uk. 5

Tahariri

# Kamwe msiutikise Muungano wetu. Komeni

MOJA ya tunu kubwa na zenye nguvu katika nchi yetu ni kuwepo kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muungano huu uliodumu kwa zaidi ya miongo sita, siyo jambo dogo la kuchezewa kwa maneno mepesi, jazba za kisiasa au chokochoko za majukwaani.

Huu ni urithi mkubwa wa kihistoria, kisiasa na kijamii uliojengwa kwa maono, busara na ujasiri wa viongozi wetu waasisi; Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

Kwa miaka mingi, Muungano huu umekuwa nguzo ya amani, mshikamano na utulivu wa nchi yetu. Wakati mataifa mengi Afrika yakipitia misukosuko ya migawanyiko, vita vya wenyewe kwa wenyewe na mapigano ya kikabila au kikanda, Tanzania imeendelea kusimama kuwa mfano wa nchi iliyochagua umoja badala ya utengano.

Uchaguzi huo kamwe siyo wa bahati mbaya; ni matokeo ya uamuzi wa kihistoria uliofanywa kwa masilahi mapana ya watu wa pande zote mbili.

Ndiyo maana Pambazuko tunasikitishwa kusikia kuanza kuibuka kwa kauli, mijadala na chokochoko zenye kuashiria nia ya kuutikisa, kuudhoofisha au hata kuumong'onyoa Muungano huu.

Inashangaza zaidi pale baadhi ya kauli hizo zinapotoka kwa watu wanaopaswa kuwa walinzi wakubwa wa masilahi ya wananchi, wakiwamo wawakilishi ndani ya vyombo vikubwa vya uwakilishi na uamuzi.

Ni kweli, yapo mambo kadhaa ya Muungano ambayo wananchi wamekuwa wakiyalalamikia na kuyapigia kelele kwa muda mrefu, haya ni masuala yanayohitaji kujadiliwa kwa uwazi, hekima na dhamira njema ili Muungano uwe imara zaidi, wa haki zaidi na wenye manufaa yanayoonekana kwa wananchi wa pande zote mbili.

Ieleweke kuwa Pambazuko tunaamini kuwa – kuwepo kwa matamanio ya maboresho, siyo sawa na kuhubiri kuvunja Muungano. Kukosoa changamoto siyo sawa na kupandikiza mbegu za chuki, mashaka na kuhimiza utengano.

Viongozi wetu wanapaswa kutambua kuwa maneno yao yana uzito mkubwa. Kauli moja ya kiongozi inaweza kujenga au kubomoa, kuunganisha au kugawa, kutuliza au kuchochea taharuki. Hivyo, wale wote wanaotumia nyadhifa zao kujaribu kuutikisa Muungano wanapaswa kuacha mara moja.

Tanzania ni kubwa kuliko tamaa za kisiasa, hasira za muda mfupi au ajenda binafsi – ambazo mara nyingi zinakuwa zimefichwa na jambo kubwa na huenda baya.

Tunachohitaji sasa siyo chokochoko, bali mjadala wa kistaarabu kuhusu namna bora ya kuimarisha Muungano wetu. Kama kuna kasoro, zirekebishwe. Kama kuna kero, zisikilizwe. Kama kuna maeneo yanayohitaji maboresho ya kisheria, kiutawala au kisera, yafanyiwe kazi kwa njia rasmi na za heshima.

Muungano huu ni nyumba yetu ya pamoja. Kazi ya viongozi siyo kuvunja kuta zake, bali kuziba nyufa zinazoonekana kuwepo kwa muda mrefu, au kuanza kuibuka sasa kutokana na mabadiliko ya mazingira.

Tunawaomba wote wenye nia ya kuuvuruga waache mara moja. Tanzania ilijengwa kwa umoja; isibomolewe kwa mihemko ya kisiasa ama tamaa binafsi za wachache ambao – wao na wanaowategemea, wamekuwa wanufaika wa Muungano huo wanauona leo kuwa ni sawa na tambala la deki.

Sisi Pambazuko tunasema; "wakome mara moja kuleta chokochoko za kuumong'onyoa Muungano huu wa mfano Afrika."

# Nimerudi nyumbani...



*Rais wa Namibia, Dkt. Netumbo Nandi-Ndaitwah (katikati), jana alipata wasaa wa kutembelea eneo alilowahi kuishi akiwa Tanzania na hapa yupo na baadhi ya majirani aliowahi kukaa nao eneo la Magomeni jijini Dar es Salaam. (Na Mpigapicha Maalum).*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na Pale

## Kagame bado yupoyupo

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, anadaiwa kutoonyesha dalili zozote dhahiri za kustaafu uongozi wa nchi hiyo, licha ya mjadala wa muda mrefu kuhusu mustakabali wake kisiasa.

Kagame (anakaribia miaka 70), ambaye ameongoza Rwanda kwa zaidi ya miaka 26, amekuwa akisisitiza kuwa uamuzi wa kuendelea au kuondoka unapaswa kuzingatia matakwa ya wananchi na masilahi ya nchi.



Hata hivyo, wapinzani wake wanasema mazingira ya kisiasa nchini humo hayatoi nafasi sawa kwa ushindani wa kidemokrasia. Wanasiasa kama Victoire Ingabire na wakosoaji wengine wamekuwa wakidai kuwa vyama pinzani vinabanwa, viongozi hukamatwa au kuzuiwa kugombea.



## Trump atamba yeye bosi

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amezua gumzo baada ya kuchelewa kuingia kwenye kikao cha viongozi wa G7 nchini Ufaransa, lakini badala ya kuomba radhi, akatania kuwa yeye ndiye "bosi".

Trump aliingia ukumbini huku viongozi wengine wakiwa tayari wameketi wakimsubiri. Alipoingia eneo la kikao, alisikika akisema, "mimi ni bosi," kauli iliyopokelewa kwa vicheko na baadhi ya viongozi waliokuwapo.

Tukio hilo limeibua mijadala kuhusu mtindo wake wa uongozi na namna anavyotumia mizaha hata katika mikutano mikubwa ya kidiplomasia.

Ingawa baadhi waliiona kauli hiyo kama utani wa kawaida, wengine wameitafsiri kama ishara ya kujiamini kupita kiasi katika jukwaa la kimataifa.



## Muhoozi azua taharuki

MKUU wa Majeshi ya Uganda, Jenerali Muhoozi Kainerugaba, amezua taharuki kubwa baada ya kuripotiwa kuhusika na kukamatwa kwa mwanasiasa wa upinzani na wakili maarufu, Erias Lukwago.

Lukwago, aliyekuwa Meya wa Jiji la Kampala na mwanasheria wa mpinzani mkongwe, Kizza Besigye, anadaiwa kukamatwa na wanajeshi nyumbani kwake wakati akijiandaa kumkabidhi Muhoozi nyaraka za mahakama kuhusu tuhuma za ukiukwaji wa haki za Besigye.

Baada ya tukio hilo, Muhoozi, ambaye ni mtoto wa Rais Yoweri Museveni, alidai mitandaoni kuhusika na kukamatwa kwake na kutoa kauli za vitisho, zikiwamo za kusababisha maumivu na hata kuua wapinzani.

Vyama vya upinzani na Chama cha Wanasheria Uganda vimelaani tukio hilo, vikisema linahatarisha utawala wa sheria.

## China kukabili zaidi roboti

CHINA imeanza kujipanga kukabili athari za ongezeko la matumizi ya roboti na akili mnemba viwandani, hatua inayotajwa kutishia ajira za kawaida katika sekta ya uzalishaji.

Kupitia mpango wake mpya wa ajira, Beijing inasisitiza sera ya ajira kwanza, ikihimiza viwanda kutumia teknolojia bila kusababisha ukosefu mkubwa wa ajira.

Serikali inataka wafanyakazi waongezewe ujuzi, hasa katika huduma, teknolojia, utengenezaji wa mashine na kazi zinazohusisha ushirikiano kati ya binadamu na roboti.

Wakati huohuo, China inaendelea kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi nje ya nchi, ikiwamo miradi ya ujenzi, biashara na ajira kwa raia wake kupitia kampuni zinazopanuka kimataifa na kusisitiza kuajiri wenzao.

Na Mzee TAI

# Baba siyo jina pekee, ni wajibu uliotukuka

NIMEFARIJIKA tena kuona ipo siku dunia huamua kuwakumbuka wakina baba, nami nikiwa miongoni mwao, tunasema; aksanteni sasa, ingawa baba ni baba, hasubiri kutambulishwa kwa siku.

Nikiwa na umri ulisonga kidogo, nimekumbana na mengi kuhusu haiba za baba; ndani ya baadhi ya nyumba, baba hukumbukwa pale tu karo inapokaribia, kodi ya nyumba inapogonga mlango, au debe la unga linapoanza kutoa sauti ya upepo.

Siku nyingine, baba anaweza kusahaulika kabisa, kana kwamba yeye ni benki inayotembea, iliyozaliwa kulipa, kusaini na kunyamaza.

Jana – Juni 21, dunia iliadhimisha Siku ya Baba Duniani. Ilikuwa siku ya kuwatakia heri baba, kuwatumia ujumbe mzuri, kuwanunulia zawadi na pengine hata kuwapikia chakula cha heshima.

Lakini ukweli ni kwamba, baba wa kweli hastahili kukumbukwa siku moja tu. Baba ni taasisi. Baba ni mhimili. Baba ni fundi asiyechoka anayejenga kuta imara za nyumba ya amani, umoja, maendeleo na mshikamano.

Baba wa kweli hufanya mengi bila kupiga kelele. Huyu ndiye mtu anayehangaika asubuhi mpaka jioni, lakini akiulizwa nani kajenga nyumba, husema; "familia tumejenga." Mtoto akifaulu kwa sababu karo imelipwa kwa jasho lake, husema; "tumehangaika kufanikisha." Chakula kikiwepo mezani, husema; "tumepata riziki."

Hapo ndipo ukubwa wa baba ulipo na kamwe siyo katika sauti nzito kutisha watoto, siyo katika kuvaa suruali ndani ya nyumba, wala siyo katika kukaa sebuleni na rimoti mkononi kama mfalme wa tamthilia.

Ubaba ni wajibu. Ubaba ni moyo wa kutoa. Ubaba ni uwezo wa kubeba mzigo mzito, kisha kuifanya familia ihisi ni safari ya pamoja. Baba mzuri haongozi familia kwa kiburi, bali kwa mfano; siyo kwa vitisho, bali kwa busara na upendo.

Lakini, tuseme ukweli kwa tabasamu lenye meno yote. Wapo wanaume ambao wakisikia Siku ya Baba, nao hujitokeza kudai zawadi. Hawa ni wale ambao majukumu yao ndani ya familia yamekimbilia kusikojulikana.

Mtoto akiumwa hawapo, karo ikitajwa wanazima simu, kodi ikifika wanageuka wachambuzi wa



hali ngumu ya uchumi. Hawa siyo baba kwa maana kamili; ni wanaume tu.

Baba anayetelekeza familia, anayekimbia wajibu, anayewafanya watoto waone mama pekee ndiye mzazi, anakosa heshima ya ubaba. Kwa sababu baba siyo cheo cha kibaiolojia pekee, bali ni daraja la maadili, ulinzi, malezi na uwajibikaji.

Baba ni ngao ya familia, lakini pia ni darasa la kwanza la nidhamu, uvumilivu na kujitoa. Familia nyingi zimesimama kwa sababu baba aliamua kuwa nguzo, siyo mtazamaji.

Baba alisimama wakati wengine walilala, akatabasamu wakati moyoni kuna hesabu, na akaendelea mbele kwa ajili ya kesho bora ya watoto wake wenye ndoto kubwa.

Kwa hiyo, kila baba anayesimama imara kwa ajili ya familia yake anapaswa kuheshimiwa. Baba anayejinyima ili wengine wapate, anayefundisha kwa vitendo, anayelinda heshima ya nyumba yake na kuunganisha familia, huyo ni hazina.

Tumpe maua yake akiwa hai. Tumwambie asante, siyo kwa kelele zake, bali kwa ukimya wake wenye matunda. Na akichoka, tumkumbushe kuwa kazi yake inaonekana, hata kama mara nyingi hatusemi.

Mimi Mzee Tai nawapa kongole wababa wote na kuwaombea heri kila uchao.

## Habari Kuu

# Oktoba 29 bado yauma




***Jengo la Ofisi ya Mtendaji Kata ya Ubungo, Dar es Salaam bado halijafanyiwa ukarabati kama lilivyokutwa jana na Kamera ya Pambazuko.***

**Na Mwandishi WETU**

SASA ni takriban miezi tisa imepita tangu miundombinu mbalimbali ilipoharibiwa wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29,2025, lakini ukarabati wake haujafanyika.

Tume ya uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa amani wakati na baada ya uchaguzi wa Oktoba 29,2025, ilieleza kuwa watu 518 waliuawa huku zaidi ya 800 wakijeruhiwa kwa risasi.

Kuhusu miundombinu, tume hiyo iliyoongozwa na Jaji (mstaafu) Mohammed Chande, ilieleza kuwa uharibifu wa vurugu hizo ulihusisha ofisi za serikali za mitaa, vituo vya polisi, vituo vya mabasi ya mwendokasi, magari ya umma na ya watu binafsi.

Novemba 24, 2025, Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba alitembelea Vituo vya Mabasi Yaendayo Haraka (Udart) na kuagiza kufanyiwa ukarabati haraka.

Dkt. Mwigulu aliahidi kuwa serikali itahakikisha hatua madhubuti zinachukuliwa ili kurejesha vifaa, miundombinu na huduma zilizokatizwa kufuatia kadhia hiyo.

Vilevile Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza fedha zilizotengwa kwa ajili ya Maadhimisho ya Siku ya Uhuru Desemba 9,2025, zitumike kukarabati miundombnu hiyo iliyoathiriwa na vurugu hizo zilizoibuka wakati wa maandamano ya Oktoba 29,2025.

Inaendelea Uk. 7



# Oktoba 29 bado...

Inatoka Uk. 6

Kutokana na hilo, timu ya Pambazuko imetembelea baadhi ya vituo vya mwendokasi katika Jiji la Dar es Salaam, lakini ukarabati mdogo tu ndiyo umeonekana kufanyika.

Kilichofanyika hadi sasa kwenye vituo hivyo ni kuweka fremu za kuwekea vioo tu, kitu ambacho ni hatari hasa kwa watoto na wanafunzi wanaotumia usafiri huo.

Katika vituo hivyo, maofisa wanaokata tiketi hawana sehemu maalum ya kukaa na kutunzia fedha na vifaa vingine vya kazi kama ilivyokuwa kabla vituo hivyo kuharibiwa.

Hivi sasa maofisa wengi wanaokata tiketi wanalazimika kukaa kulingana na mazingira ya kituo husika ili kuweza kutoa huduma kwa abiria.

Abiria, Aneth Jackson mkazi wa Kimara Bonyokwa, aliyekutwa kwenye Kituo cha Korogwe alisema changamoto ya wahudumu kutokaa sehemu zao inasababisha abiria kutofuata utaratibu wa kufuata foleni kama zamani.

Kutokana na hilo, abiria huyo aliiomba serikali kuharakisha kujenga vituo hivyo.

“Hivi mwandishi angalia jinsi huyu mhudumu alivyokaa hapo ameweka kompyuta yake juu ya box na kreti la soda ili aweze kuhudumia watu, huu siyo utaratibu mzuri wa kiofisi,”alisema Aneth.

Kwa upande wa vituo vya Polisi pamoja na ofisi za serikali mitaa vilivyopo maeneo tofauti katika Jiji la Dar es Salaam, vinaonekana kama vimetelekezwa kutokana na kutofanyiwa matengenzo yoyote hadi sasa.

Mkazi wa Kigogo, Salum Juma aliliambia Pambazuko kuwa wakazi wa eneo hilo wanapata shida ya kiusalama kutokana na kukosa huduma baada ya Kituo Kidogo cha Polisi Kigogo kutofanya kazi kwa muda mrefu.

“Huku Kigogo kuna vibaka wanafanya sana matukio ya kupora watu kwa nyakati tofauti na sasa matukio yameongezeka baada ya kukosekana kituo cha polisi,” alisema mkazi huyo.

Inaendelea Uk. 8




*Kituo Kidogo cha Polisi Kibo, bado hakijafanyiwa matengenezo kama kilivyokutwa jana na Kamera ya Pambazuko.*




*Kituo Kidogo cha Polisi Kigogo, Dar es Salaam bado hakijafanyiwa matengenezo kama kilivyokutwa jana na Kamera ya Pambazuko.*




*Kituo Kidogo cha Polisi Pasiasi, Mwanza bado hakijafanyiwa matengenezo kama kilivyokutwa jana na Kamera ya Pambazuko.*

## Habari Kuu



*Kituo Kidogo cha Polisi Kimara, Dar es Salaam bado hakijafanyiwa matengenezo kama kilivyokutwa jana na Kamera ya Pambazuko.*

# Oktoba 29 bado...

Inatoka Uk. 7

Wafanyabishara wa chakula katika eneo la Shekilago zilipo Ofisi za Serikali ya Mtaa Ubungo, wamesema kukosekana kwa ofisi hiyo, kumeleta usumbufu kwa wananchi wengi.



*Jengo la Ofisi ya Mtendaji Kata ya Nzovwe, Mbeya bado haijafanyiwa matengenezo kama kilivyonaswa na Kamera ya Pambazuko jana.*

"Hata sisi biashara siyo nzuri kutokana na wateja kupungua kwa kiasi kikubwa,"alisema mmoja wa mfanyabiashara huyo ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini.

Huko jijini Mbeya, miongoni mwa majiji ambako miundombinu yake iliharibiwa wakati wa vurugu za Oktoba 29,2025, nako hadi sasa hakuna matengenezo yaliyofanyika.

Akizungumza na Pambazuko kupitia simu yake ya kiganjani, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alisema serikali inaendelea na ukarabati wa miundombinu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Ukarabati unaendelea na unaenda hatua kwa hatua na kuhusu vituo vya mwendokasi tayari Udart iko kwenye mchakato huo wa matengenezo,"alisema Msigwa.

Katika hatua nyingine huduma za usafiri wa mabasi ya mwendokasi kwa njia ya Kinondoni-Moroco, bado haijaanza kufanya kazi tangu ilipotokea vurugu za Oktoba 29.


Takwimu za uharibifu wa mali uliotokana na vurugu za uchaguzi wa Oktoba 29,2025 zinahusisha; pikipiki binafsi 2,268, magari ya binafsi 1,642, magari ya serikali 976, ofisi za serikali, 756, vituo vya mafuta 672, nyumba binafsi 273, vituo vya Polisi 159 na vituo vya mwendokasi 27.



*Kamera ya Pambazuko juzi iliwakuta abiria wanaotumia usafiri wa mabaya ya Udart wakifanya malipo kwa wahudumu waliosimama baada ya miundombinu ya ofisi yao kuharibika kwenye vurugu za Oktoba 29, katika Kituo cha Shekilango, Dar es Salaam.*

# Mbunge ataka wizi serikalini udhibitiwe

**Na Hellen NGOROMERA**



*Mbunge wa Sikonge, Amos Maganga*

MBUNGE wa Sikonge, Amos Maganga (CCM), ameitaka serikali kuimarisha taasisi za kudhibiti wizi wa fedha.

Amesema kuwa kiasi cha fedha kinachokusanywa na ama kupokelewa kutoka kwa wafadhili, kinapaswa kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa, kubwa ikiwa ni kuchangia maisha bora kwa Watanzania.

Mbunge huyo amesema pamoja na kuwepo kwa sheria za kudhibiti wizi na rushwa, lakini bado tatizo hilo limeendelea kuwepo siku hadi siku.

"Sheria zetu tulizotunga za kudhibiti wizi zitumike ipasavyo, tumeshazungumza sana na mara nyingi kuhusu wizi, lakini ni kama bado mambo hayabadiliki sana…"

"Endapo mambo yatakuwa hivi hivi hatutakuwa tunafanya lolote, zaidi ya kukusanya fedha kisha zinavuja na kushindwa kutimiza malengo, ni vyema sasa tuimarishe taasisi zetu kuliko kuimarisha watu," amesema Maganga.

Naye mbunge wa Mbeya Mjini, Patrick Mwalunenge (CCM) ameitaka serikali kuweka kipaumbele mchango wa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi hasa waendesha bodaboda na bajaji, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, huku wakichangia kodi ya serikali.

Ametolea mfano wa madereva bodaboda na bajaji katika jimbo lake akisema wana mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi.

"Hawa watu siyo masikini kama tunavyodhani, wana mchango mkubwa na wanashika uchumi wetu. Mfano katika jimbo langu la Mbeya Mjini wapo 300,067 na wakitoa shilingi 1,000 kila mmoja kwa siku unaongelea shilingi milioni 3.1 wakati kwa mwezi ni fedha nyingi," amesema.

Kwa upande wake, Mbunge wa Hai, Saashisha Mafue (CCM) ameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwaona wafanyabiashara kuwa ni wadau wenza na siyo maadui.

"Ni vyema baadhi ya wafanyakazi wa TRA wabadili mind set (mtazamo) wawaone wafanyabiashara kama wadau wenzao na siyo maadui. Kwa dira hii unamdai mfanyabiashara elfu 60, halafu unamfungia biashara yake sasa unategemea hela ya kulipa deni ataipata wapi?" alihoji Mafue.

Khamis Majanja, mkazi wa Kijitonyama, Dar es Salaam amezungumza na Pambazuko na kuhimiza wabunge ambao leo wanaendelea na mjadala wa bajeti hiyo, kuendelea kuishauri serikali namna bora ya kukusanya kodi, huku msisitizo akiomba uwekwe kwenye matumizi yaliyokusudiwa.

Tafakuri ya Bagonza




Na Dkt. Benson BAGONZA

# Tuna msiba usiokuwa na mwili wa marehemu

MIMI ni tunda la Azimio la Arusha. Chini ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kupitia Azimio hilo, tulijenga taifa kwa sera ya Ujamaa na Kujitegemea.

Ujamaa ulishindwa, lakini katika kujitegemea tulipiga hatua kubwa. Natetea hoja yangu kama ifuatavyo;

Kwanza, tulijitegemea kifikra na kujenga kizazi jeuri kilichokuwa tayari kufa na tai shingoni. Tukasema “Fedha siyo Msingi wa Maendeleo.” Kujitegemea huanza na fikra na kuimarisha kujiamini.



Pili, hatukuwekewa masharti ili tupate fedha, bali sisi tuliweka masharti katika kupokea fedha. Rekodi yetu ya kuthamini utu na kutetea haki viliwafanya mabeberu wakose hoja. Tukavumiliwa.

Tatu, maadui zetu walikuwa mabeberu. Hivi sasa wananchi ndio maadui wa kutishwa, kupotezwa, kupigwa, kushikiwa silaha na kuswagwa. Mabeberu ni waheshimiwa tusioweza kuwaambia ukweli, bali kuwadanganya.

Nne, tulipotishwa na mabeberu tuliandamana bila kushawishiwa. Tulifundishwa uzuri wa maandamano. Sasa tunafundishwa ubaya wa maandamano.

Tano, tuliandamana kupinga ubaya au kuunga mkono msimamo mzuri. Hivi sasa wanaoandamana mioyoni ni wengi kuliko wanaoandamana barabarani. Wote wanapinga mambo yale yale ila hawaambiani.

Sita, nimepitia masharti ya Washington na Brussels nikashangaa. Yote yamo ndani ya katiba yetu. Sote tumeshindwa kuyasimamia? Vyama vya siasa, bunge letu na mahakama zetu, wako wapi mpaka viranja watoke nje kutufundisha utu, haki, na utawala bora? Ni msiba.

Saba, kama tunanyimwa fedha kwa kukiuka katiba yetu na utawala bora, je itakuwaje watakapoweka masharti ya kwao yenye sura ya dini, ndoa, familia nk?

Nane, tatizo letu kuu ni “kujifanya hakuna tatizo.” Tunajiambia eti, muungano uko imara, mauaji hayakutokea, utekaji haupo ni propoganda tu, hatuna utegemezi bali ushirikiano, rushwa haipo ni kelele za wapinzani na wivu wa kutopangwa jikoni na tunaamini tuko vizuri katika diplomasia na uchumi wetu ni bora barani Afrika. Kweli? Huku siyo kurogwa ni kujiroga.

Tisa, nina neno kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na serikali;

CCM: Mlivipongeza vyombo vilivyoleta mkwamo huu. Nashauri mkae kimya, msubiri maridhiano.

Chadema: Katiba Mpya itapatikanaje bila ukweli, uwajibikaji na maridhiano? Tamaa ya katiba mpya imekuwa kubwa kuliko ya fisi. Msijipunje.

Serikali: Acheni kulilia fedha za mabeberu. Tumepoteza jina jema na sifa kila kona. Fedha zitarudi tukisafisha jina. Mnachelewesha maridhiano kwa kuendekeza uwongo na propaganda. Watu walikufa na uchaguzi ulichafuliwa. Achana na wanaharakati kwa sababu hata ninyi ni wanaharakati wa aina nyingine. Wajibika au wajibishana tusonge mbele.

Kumi, hatujamaliza madhara ya Oktoba 29, 2025. Kuna Saba na Saba inazungumzwa. Apatikane mtu anayeamini bunduki haileti amani atukumbushe.

Ndimi za viongozi ziache kuanika ushahidi wa nia ovu ya “kupasua vichwa.” Kaeni muyajenge siyo kudanganyana.

Tambueni kuwa Washington na Brussels wametutikisa, je The Hague wakitukumbuka itakuwaje?

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***


Bati/ Mtu, Mtu Bati
HATUCHOKI!
Changia kupitia
NMB A/C NO 31910046325
ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT
CRDB A/C NO 0150764151900
UWAKILI PROJECT ELCT KAD
Mawasiliano:
0754 742 423
Askofu Benson K Bagonza

Habari

# Bajeti ya kujenga uchumi kidigitali




Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar.

Na Peter NYANJE, Dodoma

MIAKA nenda-rudi, katika kuendesha na kusimamia uchumi, fedha taslimu zimekuwa uti wa mgongo wa ustawi wa Tanzania.

Kuanzia katika masoko makubwa ya Kariakoo, Dar es Salaam na Mwanjelwa, Mbeya, vituo vya mabasi, migahawa, hadi kwenye biashara za ardhi na nyumba, pesa mkononi zimeendelea kuwa njia kuu ya malipo kwa mamilioni ya Watanzania.

Hata hivyo, serikali imeamua kuikomesha hali hiyo kupitia bajeti yake ya mwaka 2026/27 iliyowasilishwa bungeni Alhamisi iliyopita na Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar.

Kupitia hatua mbalimbali zilizotangazwa katika bajeti hiyo, serikali imeanzisha kile kinachoweza kuwa moja ya mipango mikubwa zaidi ya mageuzi ya kidijitali kuwahi kushuhudiwa nchini, yanayolenga kuanzisha safari thabiti kuelekea uchumi wa kidijitali.

Lakini, Waziri Omar ameliambia Bunge kuwa dhamira ya serikali haishii katika kuboresha mifumo ya malipo pekee.

Uchambuzi wa kina wa bajeti iliyowasilishwa bungeni na Waziri wa Fedha, Dkt. Khamis Mussa Omar, unaonyesha kuwa serikali inalenga kubadili kwa kiasi kikubwa namna Watanzania wanavyofanya miamala, kuweka akiba, kukopa, kuwekeza na hata kuwasiliana na taasisi za umma. Kiini cha mkakati huo ni kujenga uchumi imara unaotegemea teknolojia, huku ukiongeza uwazi, kupanua wigo wa walipa kodi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Iwapo hatua hizo zitatekelezwa kikamilifu, zitagusa karibu kila eneo la maisha ya kiuchumi ya Mtanzania; kuanzia jinsi mwendesha bodaboda anavyolipwa na mteja hadi namna mtu anavyonunua au kuhamisha umiliki wa ardhi na magari.

### Usimamizi wa uchumi

Waziri wa Fedha hakuficha dhamira ya serikali alipokuwa akiwasilisha bajeti hiyo bungeni na kwa kutumia lugha rahisi, alisema serikali inataka kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi na kuongeza matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali inayoweza kufuatiliwa kwa urahisi.

Sababu za hatua hiyo ni wazi, kwamba ingawa fedha taslimu ni rahisi kutumia, mara nyingi ni vigumu kufuatilia mienendo yake kwa sababu hazina tabia ya kuacha kumbukumbu.

Hali hiyo huongeza uwezekano wa ukwepaji kodi, udanganyifu wa kifedha, upotevu wa mapato na shughuli nyingine zisizo rasmi katika uchumi.

Kwa upande mwingine, miamala ya kidijitali huacha kumbukumbu zinazoweza kufuatiliwa, jambo linaloongeza uwazi na kuwajibishana.

Kwa mujibu wa wachambuzi wa uchumi, utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 unahitaji uwekezaji mkubwa katika miundombinu, viwanda, afya, elimu na teknolojia.

Inaendelea Uk. 13

# Bajeti ya kujenga...

Inatoka Uk. 12

Ili kufanikisha malengo hayo, serikali ina kazi kubwa ya kukusanya mapato na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya rasilimali za ndani.

Ndiyo maana uchumi wa kidijitali unaonekana kuwa nyenzo muhimu ya kufanikisha azma hiyo.

### Malipo ya kidijitali rasmi

Kuanzia Julai 1, 2026, shughuli mbalimbali za kiuchumi zitapaswa kutumia mifumo ya malipo ya kidijitali, kwa mujibu wa Waziri Omar.

Maelekezo ya serikali kupitia bajeti hiyo yanahusu sekta nyingi ikiwemo usafiri wa umma, mabasi yaendayo kasi, reli, vivuko, usafiri wa anga, hoteli, migahawa, utalii, shule, vyuo, vituo vya mafuta, majengo makubwa ya biashara, pamoja na biashara za magari na mali zisizohamishika. Kwa miaka mingi, sekta nyingi kati ya hizo zimeendelea kutegemea malipo ya fedha taslimu licha ya ukuaji mkubwa wa huduma za simu za mkononi na benki.

Serikali inaamini kuwa kuhamisha miamala hiyo katika mifumo ya kidijitali kutasaidia kuongeza ufanisi, kupunguza mianya ya upotevu wa mapato na kuboresha usimamizi wa shughuli za kiuchumi.

Imani hiyo inatokana pia na ukuaji mkubwa wa matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali nchini. Takwimu za bajeti zinaonyesha kuwa miamala iliyopitia mfumo wa Tanzania Instant Payment System (TIPS) ilifikia miamala milioni 651 mwaka 2025 yenye thamani ya shilingi trilioni 54.95, ikilinganishwa na miamala milioni 453 yenye thamani ya shilingi trilioni 29.82 mwaka 2024. Takwimu hizo zinaashiria kuwa Watanzania tayari wanaanza kuzoea matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali.

### Miamala ya mali nayo kidijitali

Miongoni mwa hatua zenye uzito mkubwa katika bajeti hiyo zilizotangazwa na Balozi Omar ni uamuzi wa serikali kuifanya uthibitisho wa malipo ya kidijitali kuwa sharti la lazima katika uhamishaji wa umiliki wa mali.



Waziri Omar aliliambia Bunge kuwa kuanzia Julai 1, 2026, mtu atakayehitaji kuhamisha umiliki wa ardhi, nyumba au gari atalazimika kuwasilisha ushahidi wa malipo yaliyofanyika kwa njia ya kidijitali.

Hatua hiyo inaweza kubadilisha kabisa namna miamala mikubwa inavyofanyika nchini.

Kwa muda mrefu, taasisi za serikali zimekuwa zikikumbana na changamoto ya kuthibitisha thamani halisi ya miamala ya mali kutokana na matumizi ya fedha taslimu.

Mara nyingi hali hiyo imechangia kutokuwepo kwa uwazi wa kutosha na kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.

Chini ya mfumo mpya, taasisi kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara ya Ardhi, Brela na taasisi nyingine za umma zitahitaji uthibitisho wa malipo ya kidijitali kabla ya kuridhia uhamisho wa umiliki.

Kwa mujibu wa wachumi, hatua hiyo ni miongoni mwa mifumo madhubuti zaidi ya kusimamia utii wa sheria za kodi na fedha iliyowahi kuanzishwa katika miaka ya karibuni.

Ujumbe wa serikali ni mmoja tu: hakuna rekodi ya kidijitali, hakuna uhamisho wa mali.

### Nguvu ya jamii namba

Nguzo nyingine muhimu ya mageuzi haya ni utekelezaji wa programu ya Jamii Namba kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Mpango huo unatarajiwa kuwa msingi wa kuunganisha taarifa mbalimbali za wananchi na taasisi katika mfumo mmoja.

Inaendelea Uk. 14

# Bajeti ya kujenga...

Inatoka Uk. 13

Kwa miaka mingi, serikali imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya mifumo isiyounganishwa, jambo ambalo limekuwa likikwamisha utambuzi wa watu, biashara na shughuli za kiuchumi.

Kupitia Jamii Namba, serikali inalenga kuongeza uwazi, kupunguza udanganyifu na kurahisisha utoaji wa huduma.

Kwa muda mrefu, mfumo huo unaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa sekta za kodi, benki, usajili wa biashara na hata mifumo ya hifadhi ya jamii.

Kwa wawekezaji na taasisi za fedha, mfumo madhubuti wa utambuzi wa watu na biashara hupunguza hatari na kuongeza imani katika miamala ya kidijitali.

### Uchumi usio rasmi

Labda eneo lenye uwezo mkubwa zaidi wa kuleta mabadiliko ni mkakati wa kuihusisha sekta isiyo rasmi katika uchumi wa kidijitali.

Kwa muda mrefu, matumizi ya teknolojia za kifedha yameonekana zaidi katika kampuni kubwa na maeneo ya mijini.

Sasa serikali inataka kubadili hali hiyo.

Waziri wa Fedha alifafanua kuwa mpango uliopo ni kuongeza matumizi ya Lipa Namba na QR Codes kwa waendesha bodaboda, mama lishe, wafanyabiashara wa masokoni na watoa huduma wengine wadogo.

Waziri Omar aliwaambia wabunge kuwa chini ya mwelekeo mpya, wafanyabiashara watakaopokea malipo kwa njia za kidijitali watapewa kipaumbele zaidi katika kupata mikopo inayotolewa na serikali pamoja na taasisi za fedha.

Kwa biashara nyingi ndogo, ukosefu wa mikopo nafuu ni moja ya vikwazo vikubwa vya ukuaji. Rekodi za miamala ya kidijitali zinaweza kusaidia taasisi za fedha kutathmini uwezo wa biashara na hivyo kuongeza uwezekano wa kupata mikopo.

### Kwaheri vocha za kukwangua

Hatua nyingine ya kipekee iliyotangazwa katika bajeti ni kuanza kuondolewa kwa vocha za simu za kukwangua katika maeneo ya mijini.

Ingawa kwa wengi hatua hiyo inaweza kuonekana ndogo, kwa serikali ni sehemu ya mkakati mkubwa wa kuhamasisha matumizi ya mifumo ya kidijitali hata katika shughuli ndogo za kila siku.

Kwa miaka mingi, vocha za kukwangua zimekuwa alama ya matumizi ya fedha taslimu katika huduma za mawasiliano.

Kuondolewa kwake kunaashiria mabadiliko kuelekea ununuzi wa muda wa maongezi kupitia simu, benki na mifumo mingine ya kidijitali.

### Kujitegemea kifedha

Nyuma ya kila hatua ya kidijitali iliyotangazwa kwenye bajeti kuna lengo moja kubwa zaidi: kuimarisha uwezo wa serikali kukusanya mapato na kusimamia uchumi wake kwa ufanisi zaidi.

Kwa sasa, teknolojia imekuwa silaha mpya katika mapambano ya kuongeza mapato ya ndani bila kuongeza mzigo mkubwa wa kodi kwa wananchi.

Badala ya kuongeza kodi kwa kiwango kikubwa, serikali inaelekeza nguvu katika kuboresha mifumo ya ukusanyaji na kupanua uchumi rasmi.

### Changamoto

Ni wazi kuwa safari ya kuelekea uchumi wa kidijitali haitakuwa rahisi.  Changamoto za miundombinu ya intaneti, elimu ya matumizi ya teknolojia, usalama wa mifumo ya kidijitali na upinzani kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara bado zipo.

Hadi hivi sasa ni wananchi wachache, hata miongoni mwa wanaotumia simu janja, ambao wanaielewa vizuri mifumo hiyo ya malipo.

Pamoja na hayo, rekodi zilizopo zinaonesha kuwa bado hakujawa na matumizi makubwa ya simu za mikononi, hasa katika maeneo ya vijijini, jambo ambalo litawaweka Watanzania wengi nje ya mifumo hiyo inayokumbatiwa na serikali.

Usalama wa mifumo hiyo ni jambo jingine ambalo linaweza kutatiza utekelezaji wa azma ya serikali kwa ufanisi.

Kumekuwa na matukio mengi ya wizi mitandaoni, kudukuliwa kwa akaunti na masuala mengine yanayoonesha usalama mdogo kwa watumiaji wa mifumo ya kidijitali huku serikali ikiwa haijaonesha kuwa na uwezo wa kulidhibiti suala hilo.

# Madhara uamuzi Bunge la Ulaya kwa Tanzania

**Na Mwandishi WETU**

SERIKALI imetakiwa kutodharau mchakato unaoendelea ndani ya Bunge la Jumuia ya Ulaya unaolenga kusitisha misaada kwa Tanzania.

Ushauri huo umetolewa na Mhadhiri wa Siasa na Uongozi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Richard Mbunda, baada ya Bunge la Ulaya kupitisha azimio linaloitaka Tume ya Ulaya kusitisha msaada wa Euro milioni 156 (takriban shilingi bilioni 480) kwa Tanzania.

Dkt. Mbunda amesema uamuzi wa Bunge la Ulaya siyo wa kupuuzia wala kutilia shaka kwa kuwa Jumuia ya Ulaya inafuata na kuheshimu misingi ya demokrasia na uwazi.

Akizungumza na Pambazuko, Dkt. Mbunda amesema matendo yoyote ya Tume ya Ulaya lazima yatazingatia sauti ya wabunge wa bunge hili ambao ndio wanaosimamia maslahi ya watu wanaounda jumuiya hiyo na vyombo vingine vyote vya kutoa maamuzi na kutekeleza maazimio hayo haviwezi kuwapuuza.

"Ni dhahiri kwamba kwa namna yoyote, hatua ya kuzuia ufadhili huo hata kama siyo wote, utaathiri mtiririko wa utendaji wa serikali kwa sababu hata hizi asasi za kiraia ambazo zinawezeshwa na ufadhili kutoka huko, kwa kiasi kikubwa jukumu lake ni kusaidia maendeleo ya watu na ustawi wao, ambapo ni kuisaidia pia serikali kunurisha watu wake.

"Ukikata misaada hiyo, wanaoumia ni Watanzania wa kawaida, na tumeona tangu mwaka uliopita walipoanza kuchukua hatua za aina hiyo, athari zake siyo ndogo na zinaonekana moja kwa moja, hatua hizo zinatuteteresha na zimeiteteresha serikali," alisema.



Kauli hiyo ya Dkt. Mbunda inafuatia uamuzi wa Bunge la Ulaya kupitisha azimio linaloitaka Tume ya Ulaya kusitisha msaada wa Euro milioni 156 (takriban shilingi bilioni 480) kwa Tanzania.

Hata hivyo, serikali ilitoa kauli ikiwatoa hofu Watanzania kuhusiana na hatua hiyo.

Uamuzi huo uliofikiwa unatokana na wasiwasi wa wabunge hao kuhusu masuala ya haki za binadamu, demokrasia, na mwenendo wa uchaguzi, wakitaka kuzuiwa kwa msaada huo kutokana na kile walichokieleza kuwa ni kutopata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa serikali katika kusimamia na kutekeleza haki hizo.

Katika hatua ya kujibu mtiririko wa matukio hayo, Ijumaa iliyopita, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushrikiano wa Afrikal Mashariki kilieleza msimamo na ufafanuzi wa Serikali ya Tanzania akieleza kuwa hatua hiyo ya Bunge la Ulaya ni mchakato wa ndani na siyo uamuzi wa mwisho wa Umoja wa Ulaya kuhusu programu hiyo.

Katika taarifa yake, serikali ilieleza kuwa kati ya Euro milioni 156 zilizopendekezwa, ni Euro milioni 17 pekee ndizo zilizopangwa kuingia moja kwa moja serikalini.

Kiasi kikubwa kilichobaki kililengwa kupitia mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za Umoja wa Ulaya.

Inaendelea Uk. 16



Dkt. Richard Mbunda

# Madhara uamuzi...

Inatoka Uk. 15

"Serikali imesisitiza kuwa uhusiano wa kidiplomasia na Umoja wa Ulaya bado ni imara na wa kimkakati," ilielea sehemu ya taarifa hiyo, ikiwataka wananchi kupuuza upotoshaji na kuona kuwa ushirikiano na EU bado unaendelea kunufaisha pande zote.

Lakini Dkt. Mbunda ameonya kuwa pamoja na kuwa hatua hizo ni za ndani na za kawaida, lakini matokeo yake ndiyo yataiathiri Tanzania na ingefaa iwapo serikali ingechukua hatua sasa hivi kabla suala hilo halijafikia tamati na uamuzi kutolewa.

Dkt. Mbunda alieleza kuwa kutokana na hatua hizo, tunachoshuhudia kwa sasa ni kwamba serikali imewekwa katika nafasi na hali ya kujaribu kujihami, lakini pamoja na hilo inapaswa kuchukua hatua za kuinusuru nchi kuingia katika kadhia ya kunyimwa au kufutiwa misaada na mikopo.

"Hatua hii kwanza ya kujadiliwa vile inatuingiza katika masikio ya jumuiya ya kimataifa kama watu wasio salama tena, wasiostahili kuaminiwa…"

"Hii inatuteteresha kisiasa na zaidi inatuteteresha kwa wafadhili wengine ambao tumekuwa tukishirikiana nao, kwamba linapokuja suala la Tanzania wanaanza kurejea kwenye haya yanayotokea kabla ya kufikia uamuzi…"

"Kwa hawa wadau wa maendeleo ambao wengi tunategemeana, kuna kupokea na kutoa, kwa hiyo wakishakuondolea sifa hawa ya kupokea misaada yao, wanakuondolea pia ujasiri wa kusimama na wadau wengine, wanaondoa ujasiri wa majadiliano na unaonekana kuwa una shida kila mahala kwa hiyo hustahili kuaminiwa wala kushirikiana nawe na mwisho unashindwa kupata ufadhili," alisema.

**Nini kifanyike**

Dkt. Mbunda anasema kwa Tanzania siyo ya kwanza kukutana na hali hii. Zipo nchi kadhaa zimewahi kukutana na mambo haya na misukosuko kama hii, kama ilivyowahi kutokea kwa Zimbabwe, ingawa mazingira ni tofauti kidogo.

Amesema kwa Zimbabwe kulikuwa na mshikamano mkubwa wa ndani, wananchi waliungana kuilinda serikali kutokana na namna walivyochukulia chanzo cha misukosuko hiyo na mwishowe kwa umoja wao walikuwa tayari kwa lolote kwa umoja wao.

"Bahati mbaya hapa kwetu, ninapoangalia sidhani kama kuna mshikamano wa namna hiyo hasa kutokana na haya yanayoendelea na ukitaka kujua hili fanya utafiti mdogo tu uangalie ni watu wangapi wanaunga mkono hatua hizi na kuitetea serikali.

"Katika kukabiliana na hali kama hii, kwa hatua na mambo yanavyoendelea, mshikamano wa ndani kwa sasa unaweza kuletwa na nia ya dhati ya maridhiano ambayo ndiyo pekee inaonekana inaweza kusaidia mshikamano.

"Ukiangalia mambo yanayotajwa kuhusishwa, kama suala la mazingira ya Tundu Lissu kushtakiwa na kuendelea kuwepo mahabusu, ni nani anayenufaika nalo? Kwa nini Lissu haachiwi na anaendelea kuwa ndani? Hivi suala kama hili ni hadi Marekani aje, hayo mengine yanayotajwa, je hatua zinazochukuliwa zinaonesha nia ya kuwepo maridhiano kweli?"Anahoji.

# Gharama matibabu ya figo, kansa zatisha

**Na Mwandishi WETU**



MSANII wa kizazi kipya ambaye kwa sasa anaishi nchini Marekani, Ibrahim Musa maarufu Roma Mkatoliki ameishauri serikali na sekta binafsi kupunguza gharama za matibabu ya figo na kansa.

Roma aliandika ushauri huo kwenye ukurasa wake wa Instagram huku akisisitiza kuwa gharama za afya zisiwe anasa.

Takwimu ya mwaka 2024 inaonyesha kuwa asilimia 9.1 hadi 13.1 ya watu duniani wanaishi na magonjwa mbalimbali ya figo.

Kwa upande wa Tanzania, takwimu za Wizara ya Afya – kwa mwaka 2024/25, zinaonyesha kuwa asilimia saba ya watu wanaoishi vijijini wanaishi na magonjwa ya figo na asilimia 15.5 ya watu wanaoishi mijini wanaishi na magonjwa mbalimbali ya figo.

Katika ujumbe huo wa Roma, pia aliishauri jamii kubadili mfumo wa maisha hasa kwa kuanza kukaa mbali na vyanzo vinavyosababisha maradhi hayo vinginevyo kila siku watazikwa wengi wakiwa na umri mdogo.

"Gharama kubwa za matibabu ya dialysis (kwa magonjwa ya figo), chemo (kansa), imesababisha kukatisha uhai wa ndugu zetu wengi mno. Wapo wengine nao wapo vitandani sasa wanaugulia, wengine wanatembea wakiamini ni wazima, lakini bila kujua tayari wanayo haya maradhi…"

"Siku zinavyozidi kwenda, ongezeko la waathirika wa maradhi haya linakua kwa kasi kubwa mno huku vifo vingi vikitokea kwa sababu ya kushindwa kumudu gharama na kutofika vituo vya afya mapema na kwa wakati sahihi…"

"Tutaendelea kupoteza kundi kubwa sana la wapendwa wetu kama haitafanyika jitihada kubwa kupunguza gharama za matibabu na kuongeza elimu kuhusu afya zetu na checkup mara kwa mara,"aliandika Roma na kuungwa mkono na wafuasi wengi.

Aliendelea kuandika kuwa familia nyingi zimekuwa maskini baada ya kuuza kila kitu kwa



Roma Mkatoliki

ajili ya matibabu ya ndugu zao na bado hawakupona.

"Bills (gharama) za matibabu haya unaweza ukauza kila kitu ili ujitibu na bado ukaishia njiani, pesa inakata na maradhi hayajaisha.

"Utasema uchangishe ndugu, jamaa, marafiki watachanga na itafika wakati watachoka na kuishiwa kutokana na wao kuwa na majukumu mengine pia.

"Suluhisho la haya ni serikali kuliangalia hili kwa uzito mkubwa kwa kupunguza gharama za matibabu kuliko ilivyo sasa na suala la afya lisionekane ni anasa,"alishauri msanii huyo.

Biashara

# Tacas waunga mkono ada maboresho bandari



Na Mwandishi WETU

CHAMA cha Mawakala wa Forodha Tanzania (Tacas) kimesema pendekezo la ada ya asilimia 4.5 ya Uendelezaji wa Miundombinu Bandari (PID) inalenga kusaidia maboresho makubwa na ufanisi wa huduma za usafirishaji wa mizigo.

Akizungumza mjini Mtwara hivi karibuni katika mkutano wa wadau wa watumiaji wa Bandari ya Mtwara kuhusu ada hii ya kuendeleza miundombinu mipya ya bandari, Mwenyekiti wa Tacas, Ephraim Mwankusye, alisema fedha zitakazopatikana zitaelekezwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali mipya ya kuendeleza miundombinu ya bandari za Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na maendeleo ya Bandari ya Bagamoyo pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mafuta katika bandari mbalimbali nchini.

Alisema lengo kubwa ni kuhakikisha bandari za Tanzania zinakuwa za kisasa, zenye uwezo mkubwa wa kuhudumia mizigo mingi kwa haraka na ufanisi zaidi.

Tozo hiyo ya PID ni fedha inayokusanywa kutoka kwa watumiaji wa bandari kwa ajili ya kugharamia maendeleo na maboresho ya miundombinu ya bandari nchini.

Kwa mujibu wa pendekezo hilo, asilimia 4.5 ya tozo itaelekezwa katika miradi ya kuboresha bandari, magati, reli, matenki ya mafuta pamoja na barabara zinazosaidia usafirishaji wa mizigo.

Nao wadau mbalimbali walioshiriki mkutano huo, wameunga mkono ada hiyo ya uendelezaji wa miundombinu mipya ya bandari wakisema italeta mageuzi makubwa katika kuhudumia shehena katika bandari za Tanzania.

# Sasa 'Tanzania Unforgettable' yatua Kombe la Dunia 2026



**Na Mwandishi WETU**

WAKATI macho ya dunia yakiwa Marekani, Canada na Mexico kufuatilia michuano ya Kombe la Dunia 2026, Tanzania imeamua kutumia jukwaa hilo kubwa la michezo kuitangaza nchi kupitia kampeni maalumu ya utalii na utamaduni inayobeba ujumbe wa Tanzania Unforgettable.

Kampeni hiyo inalenga kuwafikia mamilioni ya mashabiki wa soka, watalii, wawekezaji na wadau wa sekta ya safari duniani, kwa kuonesha kuwa Tanzania siyo tu nchi ya vivutio vya asili, bali pia ni lango la historia, utamaduni, vyakula, muziki, sanaa na ukarimu wa Kiafrika.

Kupitia maonyesho, matangazo ya kidijitali, mitandao ya kijamii na shughuli za kitamaduni katika miji mbalimbali yenye shamrashamra za Kombe la Dunia, Tanzania inatarajiwa kujitangaza kama moja ya maeneo bora zaidi kutembelewa baada ya michuano hiyo.

Vivutio kama Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa Serengeti, Bonde la Ngorongoro, visiwa vya Zanzibar, fukwe za bahari, hifadhi za kusini na magharibi mwa nchi, pamoja na urithi wa kihistoria wa Bagamoyo, Kilwa na maeneo mengine, vinatarajiwa kuwa sehemu ya simulizi kuu ya kampeni hiyo.

Wadau wa utalii wanasema Kombe la Dunia ni zaidi ya mashindano ya soka; ni mkusanyiko wa mataifa, tamaduni na fursa za kibiashara. Kwa kutumia mwanya huo, Tanzania inaweza kuongeza idadi ya wageni, kuvutia uwekezaji katika hoteli na usafiri, pamoja na kuongeza ajira kwa vijana katika sekta ya utalii.

Aidha, kampeni hiyo inalenga kuimarisha chapa ya Tanzania duniani kwa kuonesha taswira ya nchi yenye amani, watu wakarimu na vivutio vya kipekee visivyopatikana mahali pengine.

Kwa ujumla, Tanzania Unforgettable inabeba ujumbe mmoja mkubwa; baada ya mashabiki kushuhudia burudani ya soka Amerika Kaskazini, safari inayofuata iwe Tanzania — ardhi ya maajabu yasiyosahaulika.


Sambamba na kuitangaza Tanzania kwa njia hiyo, pia michuano mikubwa ya Mabingwa wa Soka Afrika (Afcon) inayofanyika Tanzania, nayo inapewa nafasi katika kuipaza zaidi.




*Kocha wa zamani wa klabu kubwa za Liverpool ya Uingereza na Borussia Dortmund ya Ujerumani na ambaye sasa ni Mshauri Mkuu wa Masuala ya Michezo katika kampuni ya Red Bull, Jürgen Klopp, amekutana na kampeni ya kuitangaza Tanzania katika viunga vya viwanja vya FIFA World Cup 2026 huko Marekani na kuweka alama yake.(Picha kutoka Facebook ya Dkt. Hassan Abbas)*

■ Habari

# Wanaopotosha elimu ya lishe mitandaoni kukiona



Na Mwandishi WETU

KATIKA kipindi hiki cha dunia ya kidijitali, mitandao ya kijamii imekuwa jukwaa kuu la kusambaza taarifa mbalimbali ikiwemo masuala ya lishe na afya.

Kila siku, watu binafsi, wataalamu na hata wasio wataalamu hushiriki ushauri, mapendekezo na uzoefu wao kuhusu vyakula na mitindo ya maisha yenye afya.

Hali hiyo imechangia kuongezeka kwa uelewa wa lishe kwa jamii, lakini pia imeibua changamoto kuhusu uhalali na usahihi wa taarifa zinazotolewa.

Ofisa Lishe Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Lishe na Chakula Tanzania (TFNC), Maria Ngilisho ameliambia Pambazuko kuwa siyo kila anayetoa elimu ya lishe mtandaoni ni mtaalamu.

Anasema wananchi wanapaswa kuhakiki sifa za mtoa elimu na kuzingatia taarifa zinazotolewa na wataalamu au taasisi zinazotambulika ili kuepuka kupotoshwa.

Akitoa sababu za watu wanaotoa elimu ya lishe mtandaoni kuongezeka, Ngilisho anasema wengine wana nia ya kusaidia na wengi hutoa taarifa kutokana na uzoefu wao binafsi kama vile kupunguza uzito au tiba kwa changamoto kadhaa za afya.

"Sababu nyingine ni upatikanaji rahisi wa taarifa kupitia intaneti, watu wengi wanaweza kusoma makala, kutazama video au kusikiliza vipindi vya afya na kisha kujiona wana uelewa wa kutosha kushiriki taarifa hizo…"

"Wengine wanatoa elimu hiyo kupitia mitandao ya kijamii ili kujipatia kipato, wapo pia wanaofanya hivyo kwa kutafuta umaarufu na kujipatia wafuasi"anasema mtafiti huyo.

Aidha, anasema baadhi ya watu wanaweza kuwa na maarifa ya jumla kuhusu afya, lakini wasitambue kuwa ushauri wa lishe unahitaji ujuzi maalum na mara nyingi unatakiwa kuzingatia hali binafsi ya mtu.

Mei 7,2026, Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba wakati akijibu maswali ya wabunge, alikiri kuwepo ongezeko kubwa la watu wanaotoa elimu ya afya na lishe.

Alisema jambo hilo linatokana na kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya afya pamoja na kupanuka kwa vyuo vinavyotoa taaluma hiyo nchini.

Hata hivyo, Dkt. Mwigulu alisema serikali inaendelea kusimamia sera, sheria na miongozo ya afya na lishe ili kuhakikisha wananchi wanapata elimu sahihi na salama kutoka kwa wataalamu wenye sifa zinazotakiwa.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kulinda usalama wa wananchi dhidi ya taarifa zisizo sahihi zinazoweza kuathiri afya zao.

Waziri mkuu huyo alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe ambaye alihoji kuhusu kuongezeka kwa watu wanaotoa elimu ya lishe na afya bila kuwa na utaratibu rasmi wa kitaalamu nchini. Mbunge huyo alisema wananchi wengi wamekuwa wakichanganyikiwa kutokana na elimu hiyo inayotolewa kupitia mitandao na majukwaa mbalimbali.

Inaendelea Uk. 21

# Wanaopotosha...

Inatoka Uk. 20

Wakati akichangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2026/27 bungeni Mei 12,2026, Mbunge wa Kigoma Mjini, Clayton Chipando maarufu Baba Levo, alishauri wizara hiyo kuwa na kitengo maalum kwa ajili ya kutoa elimu ya afya na lishe mitandaoni.

"Mheshimiwa mwenyekiti mimi nimekula ugali kwa miaka 35, lakini leo kila ukiingia mtandaoni utakutana na matangazo mbalimbali yanayotumika kuelimisha watu juu ya utaratibu wa matumizi ya chakula…"

"Katìka siku za hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la watoa huduma, ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakitoa elimu kuhusu lishe na kuwaweka wananchi kwenye mtanziko wa nini wale na kiwango gani,"alisema Baba Levo.



*Ofisa Lishe Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Lishe na Chakula Tanzania (TFNC), Maria Ngilisho*

**Nini kifanyike?**

Akitoa ushauri wa kudhibiti wimbi la watu wasio na utaalam wa lishe kutoa taarifa za lishe mtandaoni, Ofisa Lishe Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Lishe na Chakula Tanzania (TFNC), Maria Ngilisho anasema usajili na utambuzi wa wataalam wa lishe uimarishwe.

Anasema endapo wataalam wa lishe watasajiliwa na kutambulika rasmi itawasaidia wananchi kutofautisha kati ya mtaalamu wa lishe na mtu anayetoa maoni yake binafsi.

Akashauri zaidi kwamba serikali ianzishe na kusimamia kanuni za maudhui ya afya na lishe.

"Serikali kupitia taasisi za afya na mamlaka za mawasiliano inaweza kuweka miongozo inayotaka taarifa za afya na lishe zinazotolewa kwa umma zizingatie ushahidi wa kisayansi na maadili ya taaluma.

"Pia wataalamu wa lishe na taasisi zenye mamlaka ya lishe wanapaswa kutumia mitandao ya kijamii kwa kiwango kikubwa zaidi ili kutoa taarifa sahihi na zinazotegemea ushahidi wa kisayansi.

"Kuelimisha umma kuhusu namna ya kutambua taarifa sahihi, jinsi ya kuhakiki vyanzo vya taarifa za lishe, kuangalia sifa za mtoa taarifa, na kutambua dalili za taarifa za kupotosha au zisizo na ushahidi,"amesema.

Pia amesisitiza kuwa hatua ichukuliwe dhidi ya taarifa za upotoshaji pale ambapo taarifa za lishe zinahatarisha afya ya wananchi au zinahusisha matangazo ya uongo, mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua za kisheria au za kiudhibiti dhidi ya wahusika.

Ameshauri kuwa kuwepo ushirikiano kati ya wataalamu, vyombo vya habari, taasisi zenye mamlaka ya masuala ya lishe na mamlaka za mawasiliano zinapaswa kushirikiana kuhakikisha kuwa taarifa zinazowafikia wananchi ni sahihi, salama na zenye manufaa.

"Suluhisho si kuzuia watu kuzungumzia lishe, bali kuhakikisha kwamba taarifa zinazotolewa kwa umma ni sahihi na zinatokana na ushahidi wa kisayansi…"

"Hii inaweza kufikiwa kwa kuimarisha usajili wa wataalamu, kuelimisha umma kuhusu vyanzo vya taarifa vinavyoaminika na kuongeza uwepo wa wataalamu sahihi wa lishe kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii,"ameshauri mtafiti huyo.

■ Makala

# Wema Sepetu akumbana na gharama iliyofichika ya ukatili wa mtandaoni



Na Dkt. Rose REUBEN

TAKRIBANI miongo miwili sasa, mlimbwende, muigizaji na msanii wa Tanzania, Wema Sepetu ameishi chini ya mwamvuli usio na huruma wa umaarufu.

Tangu alipotangazwa kuwa Miss Tanzania mwaka 2006, jina lake limekuwa sehemu ya watu maarufu Afrika Mashariki.

Alitoka kwenye majukwaa ya urembo na kuingia kwenye uigizaji, ujasiriamali, burudani na ushawishi kupitia mitandao ya kijamii. Kwa wengi, yeye ni mtu maarufu. Kwa wengine, ni alama ya urembo, uimara, mijadala, kujijenga upya na ustahimilivu.

Baada ya miaka mingi ya minong'ono ya umma, alipewa majina ya kuumiza na maoni yasiyoisha mtandaoni kuhusu safari yake ya kupata mtoto, hivyo kujifungua mtoto wa kiume - hivi karibuni, kwa Wema Sepetu kumekuwa zaidi ya habari ya mtu maarufu.

Lakini nyuma ya mvuto, vifijo na nderemo, vichwa vya habari na mamilioni ya miitikio mtandaoni, kuna ukweli mchungu ambao wanawake wengi viongozi au maarufu hukutana nao; uwanja wa mapambano.

Kwa wanawake kama Wema, mitandao ya kijamii siyo tu eneo la kuonekana, kujitangaza, kufanya biashara au kuunganishwa na watu, pia ni eneo ambako matusi, uvumi, udhalilishaji wa mwili, taarifa za uongo na mashambulizi binafsi vinaweza kusambaa ndani ya dakika chache.

Chapisho moja linalomhusu linaweza kuvutia maelfu ya maoni; baadhi yakiwa ya kuunga mkono, lakini mengine yakiwa ya kikatili; ya kudhalilisha na yenye madhara makubwa.

Hii ni sehemu iliyofichika wa ukatili wa kijinsia unaowezeshwa na teknolojia, aina ya ukatili unaozidi kuwalenga wanawake kupitia simu, mitandao ya kijamii, programu za ujumbe mfupi, blogu na maeneo mengine ya kidijitali.

Safari ya Wema mbele ya umma inaonesha jinsi wanawake maarufu mara nyingi wanavyochukuliwa kama mali ya umma. Miili yao hujadiliwa bila heshima. Uhusiano wao huhukumiwa bila huruma.

Mapambano yao binafsi hugeuzwa burudani. Makosa yao hukuzwa, huku mafanikio yao yakipunguzwa au kupuuzwa.

Katika zama za kidijitali, umaarufu wa mwanamke unaweza kugeuzwa kirahisi kuwa silaha dhidi yake.

Ukatili wa mtandaoni dhidi ya wanawake mara nyingi hautambuliwi kama ukatili. Watu wengi hupuuza kwa kusema ni "maoni tu," "maisha ya kawaida ya mtu maarufu," au "gharama ya kuwa maarufu." Lakini maneno yanaweza kujeruhi. Uvumi wa uongo unaweza kuharibu heshima ya mtu.

Mashambulizi ya mtandaoni yanaweza kuathiri afya ya akili, mahusiano ya kifamilia, fursa za kibiashara, kujiamini mbele ya umma na usalama binafsi.

Kwa wanawake waliopo katika tasnia ya burudani, ukatili huu mara nyingi huwa wa kijinsia. Hawashambuliwi tu kwa kile wanachofanya, bali kwa sababu ya wao kuwa wanawake.

Wanahukumiwa kwa mavazi yao, maumbo yao, umri wao, uzazi, mahusiano, hali ya ndoa, uwezo wa kupata watoto na maamuzi yao binafsi.

Aina hii ya ukatili inaakisi tatizo pana la kijamii ambapo wanawake wanatarajiwa waonekane, lakini wasiwe na nguvu kupita kiasi; wapendwe, lakini wasiwe huru; wafanikiwe, lakini bado wadhibitiwe na matarajio ya jamii.

Inaendelea Uk. 23

# Wema Sepetu...

Inatoka Uk. 22

Uzoefu wa Wema Sepetu unaakisi hali wanayopitia wanawake wengi wakiwemo waandishi wa habari, wanasiasa, wanaharakati, wasanii, wanafunzi na wajasiriamali wa kidijitali, siyo Tanzania pekee bali duniani kote.

Wanawake wanapoonekana mtandaoni, mara nyingi hukutana na mashambulizi ya kupangwa yenye lengo la kuwaaibisha na kuwanyamazisha.

Hili si suala la mtu binafsi tu. Ni suala la usawa wa kijinsia. Ni suala la uhuru wa kujieleza. Ni suala la maadili ya vyombo vya habari. Pia ni suala la haki za kidijitali.

Mwanamke anapodhalilishwa hadi kujiondoa kwenye mitandao, jamii hupoteza sauti yake. Mwanahabari mwanamke anapotishiwa kwa kuripoti ukweli, umma hupoteza taarifa.

Mwanasiasa mwanamke anaposhambuliwa kwa matusi ya kingono, demokrasia hupoteza ushiriki sawa. Msichana anapotishwa kwa picha zake binafsi, elimu, utu na maisha yake ya baadaye vinaweza kuwa hatarini.

Ukatili wa mtandaoni hauishii mtandaoni. Huwafuata wanawake majumbani, kazini, kwenye familia na kwenye jamii zao.

Kwa watu maarufu, madhara yanaweza kuwa makubwa zaidi kwa sababu maisha yao hufuatiliwa kila wakati. Uvumi kuhusu mtu maarufu unaweza kusambaa haraka kuliko ukweli.

Habari ya uongo inaweza kuwafikia maelfu kabla haijakanushwa. Kauli ya kikatili inaweza kusambazwa, kuchekwa na kurudiwa hadi ikawa sehemu ya kumbukumbu ya umma.

Ndiyo maana simulizi ya Wema Sepetu haipaswi kuchukuliwa kama udaku wa burudani pekee. Inapaswa kufungua mjadala mzito wa kitaifa kuhusu namna Tanzania inavyowalinda wanawake na wasichana katika maeneo ya kidijitali.

Teknolojia imewapa wanawake nyenzo muhimu za kujenga taaluma, kuzungumza, kuhamasisha jamii, kuuza bidhaa, kubuni kazi za sanaa na kusimulia hadithi zao. Lakini bila usalama, haki na uwajibikaji, teknolojia hiyo hiyo inaweza kutumika kuwanyamazisha, kuwaaibisha na kuwaumiza.

Kuna haja ya kuongeza uelewa wa umma kuhusu Ukatili wa Kijinsia Unaowezeshwa na Teknolojia. Wanawake na wasichana wengi hawajui wapi pa kuripoti ukatili wa mtandaoni. Wengine huogopa kulaumiwa. Wengine huhofia kuwa kuripoti kutawaweka katika hatari zaidi. Wengine hushauriwa wapuuze tu ukatili huo, hata pale vitisho vinapokuwa vya hatari.

Ukimya huu huwalinda watuhumiwa na watendaji wa ukatili.

Tanzania inahitaji mifumo imara ya kuripoti inayomlinda muathirika, elimu ya usalama wa kidijitali, uripoti wenye uwajibikaji wa vyombo vya habari, na ushirikiano bora kati ya vyombo vya dola, wadhibiti, asasi za kiraia, shule, na watumiaji wa majukwaa ya teknolojia.

Watumiaji awa majukwaa ya kijamii mitandaoni wanapaswa kuepuka kukuza uvumi wenye madhara au kuchapisha habari zinazowadhalilisha wanawake na kuelewa kuwa uhuru wa kujieleza haumaanishi uhuru wa kudhalilisha.

Familia na jamii pia zina wajibu. Badala ya kuwalaumu wanawake wanaolengwa mtandaoni, zinapaswa kuwatia moyo. Badala ya kucheka machapisho ya kikatili, watumiaji wanapaswa kuyaripoti. Badala ya kusambaza maudhui yenye madhara, watu wanapaswa kuyakatisha mzunguko wake.

Simulizi ya Wema Sepetu inatukumbusha kuwa wanawake walio mbele ya macho ya umma ni binadamu kwanza kabla ya kuwa watu maarufu. Wana hisia, familia, utu na haki. Kuonekana mbele ya umma hakupaswi kumaanisha kufanyiwa ukatili hadharani.

Dunia ya kidijitali haipaswi kuwa mahali ambapo wanawake wanaadhibiwa kwa kuonekana. Mtandao salama si suala la teknolojia pekee. Ni suala la haki, heshima, uwajibikaji na usawa.

Umaarufu unapogeuka uwanja wa mapambano, jamii lazima ijiulize: je, tunatumia teknolojia kuwawezesha wanawake, au tunairuhusu iwe silaha nyingine dhidi yao?

Jibu la swali hilo ndilo litakaloamua kama maeneo ya kidijitali yatakuwa majukwaa ya fursa au viwanja vya ukatili.

Kwa Wema Sepetu na wanawake wengine wengi, ujumbe uko wazi: ukatili wa mtandaoni si burudani. Ni ukatili. Na lazima ukomeshwe.

***Mwandishi wa makala haya ni Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa).***



■ Kilinge cha Mawasiliano

Na Loth MAKUZA

# Ushawishi: Soko lenye watu wanne

KATIKA ukumbi mmoja jijini baada ya mkutano mzito wa wadau wa mawasiliano, nilipata bahati ya kukaa pembeni na kijana mmoja aliyekuwa amemaliza chuo kikuu hivi karibuni.

Alikuwa na shahada nzuri mkononi, mtanashati na swali moja zito ndani ya kifua. Aliniuliza kitu ambacho mara nyingi vijana wa fani ya Mawasiliano na Umma (PR) huniuliza: "Mkuu, nifanyeje ili nionekane? Nifanyeje ili nipate ushawishi?"

Nikamwambia, kama ilivyo katika mpira, hata katika ofisi kuna namna nne tu za kucheza mchezo wa ushawishi.

Ukichagua mtindo wako vibaya, unaweza kucheza dakika tisini nzima bila kugusa mpira. Ukichagua vizuri, unaweza kuwa mchezaji wanayemtafuta wote.

Tatizo ni kwamba watu wengi hawajui kuwa wamechagua mtindo, wanadhani tu ndivyo walivyo kumbe kuchagua ni kuamua na kuamua ni kupanga maisha yako yote ya kikazi.

Kuna mtu mkimya au mnyamavu; huyu ni yule mtu mwenye akili, uwezo, hoja nzito kichwani, lakini hoja zile zinafia humo kichwani, anaogopa mgogoro au kupingana.

Akiwa kwenye kikao, anasubiri wengine waseme na yeye anaitikia kichwa tu. Maoni yake mazuri yanazikwa chini ya ukimya wake. Ukimuuliza, atasema "ipo sawa tu", hata kama moyoni ana dhoruba.

Tatizo la mnyamavu siyo uwezo. Mnyamavu mara nyingi ndiye mwenye akili kuliko wote chumbani. Tatizo lake ni kwamba mwajiri hawezi kupandisha cheo sauti asiyoisikia. Mteja hawezi kumkabidhi kazi mtu asiyemfahamu mawazo yake.

Mwisho, mkimya anabaki nyuma ya pazia, akifanya kazi nzito, huku sifa zikienda kwa mtu aliyeongea zaidi ya alivyofanya.

Katika mpira, huyu ni yule beki mzuri ambaye hakuna anayemkumbuka jina lake mpaka siku anapokosea.

Pia, yupo mbabe; huyu ni anajaza chumba sauti yake, anaongea juu ya wengine, anadakia kabla hujamaliza na ana hakika kwamba mawazo yake ndiyo yenye mashiko.

Kwa muda mfupi, mbabe anaonekana kiongozi, ana msimamo, ujasiri, anajua anachotaka. Kikao kinatawaliwa na yeye.

Fikiria mbabe akiwa mbele ya mwandishi wa habari wakati wa kashfa, au mbele ya mteja mkubwa siku ya mvutano. Yule mbabe anakuwa hatari kwa taasisi yenyewe.

Aidha, yupo mnafiki wa kimyakimya; huyu ndiye mgumu kuliko wote kumtambua, na ndiye hatari kuliko wote kazini, anafanana na mkimya kwa nje, haongei wazi, haonyeshi hasira moja kwa moja, lakini ndani yake kuna moto unaowaka taratibu.

Hasemi "sikubaliani" badala yake atakuwepo kwenye kikao aking'ata meno, akitoa kejeli ndogondogo, au akinyamaza kimya cha kuadhibu.

Huyu hapingani na wewe usoni; anapingana na wewe mgongoni. Hisia mbaya hazitoki kinywani mwake, zinatoka kwenye matendo yake.

Yupo mwenye msimamo; huyu ndiye mhimili wa soko, mwenye msimamo anajieleza kwa ujasiri, lakini pia anasikiliza wengine kwa makini. Anasema anachokiamini bila woga na bila dharau.

Anaweka mipaka wazi, anatamka matarajio yake bila kuzunguka na hufanya hivyo kwa heshima, sauti tulivu, macho yanayokutana na ya mwenzake, mazungumzo ya wazi na ya ukweli.

Huyu ndiye sarafu ya soko letu, huyu ndiye anayeajiriwa zaidi. Watoa uamuzi wanamwamini na wateja, wanamwamini na timu nzima. Kwa nini? Kwa sababu anaweza kupingana na hoja yako bila kukuvunjia heshima.

Kupanga ni kuchagua

Nilimaliza kumweleza kijana wangu kwamba mitindo hii minne hazaliwi nayo, inachaguliwa, mara nyingi bila kujua na mara nyingi tunaichagua kwa woga, tunanyamaza kwa kuogopa mgogoro, tuna u-babe kwa kuogopa kuonekana wanyonge, tunakuwa wanafiki kwa kuogopa kusema ukweli usoni.

Soko la ushawishi lina wateja wanne, lakini mnunuliwa wa kudumu ni mmoja. Wengine watapita, watang'aa kwa dakika, watajaza vyumba sauti zao na kejeli zao na ukimya wao.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhu- siano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***



Na Emmanuel JACOB

# Zingatia haya mwili unapopata uchovu

SAA 11 alfajiri, alarm yangu inalia, ninajivuta kweli yaani mwili wangu ni kama umemwagiwa zege. Siyo kama kawaida, kila kiungo kinauma.

Nikifika ofisini, najilazimisha, hata baada ya kikombe cha chai au kahawa hali huwa mbaya. Macho yako kwenye kompyuta, lakini akili imeganda kama barafu, sina umakini tena, natumia muda mrefu kukamilisha kazi ndogo – hali hii inajulikana kitaalamu kuwa ni 'brain fog.'

Boss hanielewi kabisa, kila mtu ofisini anaona mimi ni mzembe, lakini ukweli ni kwamba hata mimi sielewi ni nini kimenipata, ni kama napigana vita ya ndani kwa ndani na adui asiyeonekana.

Hii ni kauli ya mgonjwa aliyenieleza hali anayopitia kwa sasa, ghafla nikawaza kuhusu chronic fatigue syndrome.

Chronic fatigue syndrome ni nini hasa? Inawezekana wengi wetu wanapitia hali hii na wanadhani ni uchovu kwa sababu ya kazi, utakwisha ukilala saa za kutosha na ukiamka mzima kabisa. Ukweli ni kwamba mtu anayepitia hali hii usingizi siyo suluhisho.

Huu ni ugonjwa wa muda mrefu ulioathiri mifumo mingi ya mwili, ikiwemo mfumo wa ufahamu (central nervous system) na kinga ya mwili. Uchovu huu hauishi kwa kupumzika, hali huzidi kuwa mbaya baada ya kufanya kazi ndogo tu ya akili au inayohusisha nguvu.

### Dalili zinaonyesha ni CFS

Uchovu uliokithiri, na unadumu kwa kipindi cha miezi sita bila sababu ya ugonjwa mwingine.

Maumivu kila mahali, misuli na viungo navyo huuma bila hata kufanya kazi yoyote ya nguvu. Inaweza kuambatana na homa, au mafua mara kwa mara yanayopelekea hali inakuwa mbaya zaidi. Usingizi hausaidii, unaweza kulala hata saa 10 lakini utaamka ukiwa umechoka zaidi.

Katika ulimwengu wa ushindani wa kibiashara "kuchoka" kunatafsiriwa kama ukosefu wa nidhamu au uvivu. Mabosi wengi hawajui sana kuhusu hali kama hizi. Wanatarajia ripoti ziwe tayari kwa wakati, mikutano ihudhuriwe na tabasamu liwepo kila wakati.

"Niliambiwa na boss wangu kuwa nina tabia mbaya na sina hamasa ya kazi, kumbe nilikuwa na maumivu makali ambayo sikuwa hata na nguvu ya kujitetea" – mfanyakazi huyu aliniambia

Swali la msingi unapambanaje ukiwa kwenye hali hii?

Pangilia kazi zako; usijaribu kufanya kazi zote kwa mpigo. Hakikisha unafanya kazi ngumu pale unapoona una nguvu, lakini ni muhimu kupumzika japo kwa dakika chache, na nyoosha mwili na mazoezi mepesi.


Fanya kazi ndogo na zikamilishe itakusaidia kuwa na motisha ya kuendelea na kupambana hatua kwa hatua. Jifunze kusema hapana pale ambapo unaona hutaweza kumudu, kuwa mkweli sema huwezi, na huna nguvu kwa siku hiyo, au tafuta msaada.

Zingatia lishe bora; Punguza sukari na vyakula vya wanga vilivyosindikwa (hivi hushusha nishati kwa wingi). Kwa mbadala tumia matunda na maji ya kutosha.

Mazoezi husaidia kukabiliana na hali hii. Ninavyosema mazoezi si mazoezi mazito ya nguvu (heavy gym workout), mazoezi yasipoongozwa na mtaalamu hupelekea kuchoka zaidi na hukatisha tamaa usiendelee. Mbinu kama "graded exposure therapy" mazoezi mepesi yanayoongezeka viwango kwa hatua ndogo ndogo, husaidia kuchochea homoni za furaha na nishati (endophins).

Lengo la mazoezi siyo kuchosha mwili zaidi, bali kuuaminisha mwili wako polepole kuwa bado unaweza kuzalisha nishati na kujifunza mbinu mbalimbali zitakazokufanya umudu kazi zako kwa siku.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Ameandika Kitabu cha Mbinu za Kutibu Maumivu Sugu). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob***



Bustani ya Sheria



Na Karim Gabriel Mussa

# Simulizi ya kisheria; Kesi ya Mwamwindi kuua mkuu wa mkoa

MIONGONI mwa kesi zilizotikisa historia ya Tanzania ni ile ya Saidi Abdallah Mwamwindi dhidi ya Jamhuri, iliyotokana na mauaji ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Dkt. Wilbert Klerruu, yaliyotokea Desemba 25, 1971 katika eneo la Ismani, Iringa.

Wakati huo serikali ilikuwa ikihamasisha sera ya vijiji vya ujamaa, hatua iliyozua mvutano kati ya viongozi wa serikali na baadhi ya wakulima wakubwa waliopinga kuhamia vijijini. Mwamwindi alikuwa mmoja wa wakulima hao.

Siku ya tukio, Dkt. Klerruu alikuwa akikagua utekelezaji wa sera hiyo. Alifika katika shamba la Mwamwindi na kumkuta akiendelea kulima.

Kwa mujibu wa ushahidi wa mashahidi, mkuu huyo wa mkoa alimwamuru dereva wa trekta kusimamisha kazi na kumtaka Mwamwindi aondoke katika shamba hilo, akimkosoa kwa kile alichokiona kuwa ni tabia za kibepari.

Mwamwindi alidai kuhisi kudhalilishwa mbele ya wafanyakazi wake. Baada ya kudai kudhalilishwa zaidi, mshtakiwa alikwenda nyumbani kwake, akachukua bunduki ya mawindo na kumfyatulia risasi mbili Dkt. Klerruu, moja kifuani na nyingine kichwani, na kusababisha kifo chake papo hapo.



Ilidaiwa mahakami hapo kwamba baada ya mauaji hayo, Mwamwindi alichukua mwili wa Dkt. Kleruu na kuupakia ndani ya gari na kisha alipeleka mwili wa marehemu katika Kituo cha Polisi Iringa na kujisalimisha.

Katika kesi iliyosikilizwa na Mahakama Kuu Iringa mwaka 1972 mbele ya Jaji Onyiuke, J., Mwamwindi hakukanusha mauaji hayo, bali alidai alichochewa na hasira kali (provocation) kutokana na kudhalilishwa hadharani.

Mahakama ilikataa utetezi huo. Jaji alieleza kuwa sheria hukubali udhaifu wa kibinadamu, lakini haiwezi kuhalalisha ukatili. Alisisitiza kuwa kulikuwa na muda wa kutosha kwa mshtakiwa kutuliza hasira zake kwani aliondoka eneo la tukio, akaenda nyumbani, akachukua bunduki na kurejea kabla ya kufyatua risasi.

Kitendo hicho kilionekana kuwa kisasi kilichofanywa kwa makusudi na siyo mwitikio wa hasira za ghafla za binadamu baada ya kuhisi kutotendewa haki.

Mwamwindi alitiwa hatiani kwa kosa la mauaji chini ya Kifungu cha 196 cha Kanuni ya Adhabu na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa. Rufaa yake katika Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki ilitupiliwa mbali, hivyo hukumu ya awali kusimama na hadi kutekelezwa kwake.

Kesi hii imeendelea kuwa rejea muhimu katika sheria ya jinai nchini, ikifundisha kuwa hasira siyo kinga dhidi ya uwajibikaji wa jinai, na kwamba mtu anayepata muda wa kutafakari kabla ya kutenda hatari hawezi kutegemea utetezi wa provocation.

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***

# Siyo kosa kuteua ndugu – Sekretarieti ya Maadili


*Jaji Sivangilwa Mwangesi*

Na Mwandishi WETU

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imesema siyo kosa kisheria kwa kiongozi mwenye dhamana kuteua ndugu, jamaa au marafiki kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Uteuzi huo hauwezi kuwa kosa kisheria iwapo utazingatia sifa za mtu anayeteuliwa, wamesema maofisa wa tume hiyo wakati wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria ndani ya sekretarieti hiyo, Emma Gerani aliwaambia wahariri kuwa kosa linaweza kuwepo iwapo uteuzi huo utafanywa kwa upendeleo unaozingatia uhusiano kati ya mteuzi na mteuliwa.

Gerani alitoa ufafanuzi huo wakati akijibu swali lililoulizwa na mwandishi wa Pambazuko aliyetaka kujua sheria inasemaje kuhusiana na hatua ya baadhi ya viongozi wenye dhamana kuteua ndugu, jamaa na marafiki katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Katika ufafanuzi wake, Gerani alisema kuwa watoto, ndugu, jamaa na marafiki wa viongozi nao wana haki ya kushika nafasi za uongozi ikiwa wana sifa za kushika nafasi hizo.

Hivyo, alifafanua, iwapo watateuliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi huku wakiwa na sifa, hata kama wana uhusiano wa kindugu na anayewateua, uteuzi wao hauna mawaa kisheria.

Mwandishi wa Pambazuko aliuliza swali hilo kufuatia malalamiko mitandaoni kuhusu baadhi ya viongozi wenye dhima kuteua ndugu na jamaa kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Aidha, kumekuwepo na malalamiko kuhusu watoto wa viongozi kupata kazi katika baadhi ya taasisi za umma.

**Kuhusu zawadi**

Katika mada yake awali, Gerani aliwaambia waandishi wa habari kuwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inakataza kiongozi kupokea zawadi ambayo thamani yake inazidi shilingi 200,000 na kukaa nayo.

"Kiongozi wa umma anapopokea zawadi ambayo thamani yake inazidi shilingi 200,000 anatakiwa kuiwasilisha zawadi hiyo kwa ofisa masuuli wake na kuitolea tamko," alisema Gerani.

Kwa mujibu wa mwanasheria huyo, kifungu cha 12(1) cha sheria kinapiga marufuku kwa viongozi wa umma kujipatia manufaa ya kifedha na kwa kipekee kifungu cha 12(1)(e) kinazuia viongozi kuomba ama kupokea zawadi zenye manufaa makubwa kiuchumi.

Anasema sheria inaruhusu zawadi ambazo ni za ukarimu wa kawaida kama vile kalamu au kalenda, zawadi kutoka kwa ndugu wa karibu wa kiongozi na zawadi za ukarimu wa kitamaduni.

Inaendelea Uk. 31

Habari

# Siyo kosa kuteua ndugu – Sekretarieti...

Inatoka Uk. 30

Akifafanua, Gerani alibainisha kuwa zawadi inamaanisha kitu anachopewa mtu bila malipo yoyote kama ishara ya upendo, wema, shukrani, heshima, pongezi au kumbukumbu ya tukio fulani. "Zawadi inayokubalika kimaadili ni ile ambayo haina dhamiri ya kuathiri uamuzi au jambo lolote, mtu anatoa kwa hiari siyo kwa sababu anataka ufanyiwe jambo fulani," alisisitiza.

**Kutoa tamko**

Gerani amesema iwapo kiongozi atapokea zawadi yenye zaidi ya shilingi 200,000 atatakiwa kuitangaza mara moja.



*Wanawake wanaofanya biashara ya kukodisha viatu (Gumboot) kwa wateja wanaofuata mahitaji - hasa wakati wa vipindi vya mvua katika Soko la Mabibo, Dar es Salaam, jana wamekuwa wakiendelea kuhudumia wananchi kufuatia kuwepo kwa ubovu wa miundombinu katika soko hilo. Ni muda mrefu sasa wahusika wameshindwa kuwajibika ili kuondoa kadhia hiyo. (Picha na Kamera ya Pambazuko).*

"Ofisa Masuuli akishapokea zawadi hiyo atawasilisha tamko na kutoa uamuzi wa jinsi zawadi itakavyotumika. Atatoa tamko hilo kwa Kamishna wa Maadili.

Aidha, Gerani alisema kiongozi haruhusiwi kupokea zawadi yoyote hata kama thamani yake ni pungufu ya shilingi 200,000 iwapo zawadi hiyo inaathiri ama itaathiri uadilifu wake au utekelezaji wa majukumu yake na itasababisha kuashiria mazingira ya mgongano wa maslahi.

Akifungua kikao hicho awali, katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu wa Idara ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma, Kamishna wa Maadili, Jaji (stahiki) Sivangilwa Mwangesi, aliwataka wahariri nao kujiuliza swali la msingi la namna wanavyochangia kukuza uadilifu nchini kupitia vyombo vyao wanavyovifanyia kazi.

"Je, kuna vitendo vyovyote vya ukiukwaji wa maadili anavyokutana navyo (mhariri) katika utekelezaji wake wa majukumu? Naomba kila mmoja wetu ajitatafakari, katika utendaji wake wa kazi anasaidiaje kukuza maadili ya viongozi?

"Zipo njia mbalimbali tunazoweza kushirikiana kupeana taarifa dhidi ya viongozi wa umma wanaotuhumiwa kukiuka maadili," alisema.

Aidha, alimtaka kila mhariri kujitathimini ni kwa namna gani anatumia weledi wake kukuza maadili ya viongozi wa umma nchini, kwa sababu kazi hiyo ni ya kila mmoja wao.

Sekretariati ya Maadili ya Umma iliandaa mkutano huo ili kuwaleta pamoja na kuwa na sauti moja katika kukuza uadilifu miongoni mwa viongozi wa umma nchini.

"Ikumbuke kuwa uadilifu wa viongozi wa umma una manufaa makubwa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo katika taifa letu…"

"Taifa lenye viongozi waadilifu, rasilimali zake zinanufaisha jamii nzima. Kinyume chake rasilimali za nchi zinakuwa mikononi mwa kundi la watu wachache…"

"Hali hii husababisha manung'uniko, upendeleo na mgawanyo wa rasilimali usiozingatia mizania ya usawa," alisema.



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Hospitali za serikali zinakosaje huduma muhimu?

**Mhariri,**
MARA nyingi najiuliza, lakini sipati majibu. Hivi ni kweli hospitali zetu za serikali zinakosa dawa, wauguzi na madaktari wa kutisha?

Nasema hivyo kwa sababu imekuwa ni jambo la kawaida kwenda kwenye hospitali za serikali kutibiwa na kuambiwa dawa zimeisha.

Tunashindwa kuelewa usimamizi ndiyo mbovu au tatizo ni nini hasa?

Sasa kama jiji kubwa kama la Dar es Salaam hospitali zake hazina dawa, vipi hali ya hospitali huko mikoani?

Mamlaka husika tunaomba jambo hili mlishughulikie kwa sababu linatia aibu taifa letu.

**Manka Dustan,**
**Tabata Mawenzi,**
**Dar es Salaam.**

## Malori yatengewe muda wa kusafiri

**Mhariri,**
SISI watumiaji wa barabara tunakerwa na madereva wa malori ambao wanasababisha foleni barabarani mara kwa mara.

Hali hiyo imekuwa kikwazo kikubwa kutokana na malori hayo 'kurundikana' barabarani na kusababisha adha kubwa kwa wasafiri hasa nyakati za jioni.

Kuna wakati tunapoteza muda mwingi kwenye foleni huku tukishindwa kutimiza majukumu yetu ya kujipatia riziki.

Tunaomba mamlaka husika ilishughulikie suala hili kwa malori hayo kutengewa muda maalumu wa kusafiri, ikiwezekana kuanzia usiku wa manane hadi alfajiri.

**Mwananchi,**
**Ilemela, Mwanza.**

## Uongozi Kibaha wafafanue fedha za barabara

**Mhariri,**
HALMASHAURI ya Manispaa ya Kibaha, Pwani imesema mwaka wa fedha 2025/26 ilitumia kiasi cha shilingi milioni 420 katika kata 14 na kila moja ilipata shilingi milioni 30 kuboresha barabara za mtaa na vivuko.

Lakini, kwetu kutoka Sheli-Mpiji na ile ya Tankini-Muheza ni mbovu sana, sikumbuki mwaka waliopitisha greda japo kukwangua tu.

Barabara hizo zina mabonde na mashimo mengi, wakati wa mvua hazipitiki kabisa, kwa ufupi Kata ya Mailimoja walichofanya ni kukwangua ile njia fupi inayoelekea katika shule mpya iliyozinduliwa wakati wanapitisha mwenge tu.

Sasa tunaposikia eti shilingi milioni 30 zimetumika kuboresha miundombinu, labda Mkuu wa Mkoa wa Pwani, mbunge, mkuu wa wilaya ya Kibaha na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kibaha watueleze vizuri kuhusu matumizi ya fedha hizo zimetumikaje

**Mwananchi Mailimoja,**
**Kibaha**

Habari

# Mama Mkapa akerwa wazazi kushindwa kulea watoto



Mama Mkapa

**Na Mwandishi WETU**

MJANE wa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, Mama Anna Mkapa ameeleza masikitiko yake kwa namna wazazi wa sasa wanavyolea vibaya watoto wao.

Kutokana na hilo, amewataka wazazi nchini kuhakikisha wanawalea watoto wao kwa kuwafundisha maadili ya Kitanzania.

Mjane huyo wa Rais Mkapa, amesema hilo litasaidia kulinda utamaduni na heshima ya taifa katika kipindi hiki cha utandawazi na matumizi makubwa ya mitandao ya kijamii.

Mama Mkapa aliyasema hayo wiki iliyopita wakati akizungumza katika Siku ya Mtoto wa Afrika Juni 16, 2026.

"Unajua mimi sasa ninalea wajukuu, lakini hivi sasa hatuwapi watoto majukumu ya kutosha, tunawaachia wacheze na simu, TV hapo ndiyo tumejua tumelea…"

"Sisi tulikuwa tunaamka asubuhi sana na mtoto wa kike kule kwetu kaskazini, unapoamka asubuhi unajua kazi yako ni nini kabla hujaenda shule na unawahi shule saa moja hapo umeshafanya kazi zote za nyumbani…"

"Lakini sasa hivi utamwamsha mtoto anakuta chai tayari mezani anapakiwa kwenye gari anaenda shule, sisi ilikuwa unatembea kwenye baridi kwenye mvua kwenye jua,"alisema.

Amesema hilo kwa sasa halitokei bali watoto wanalelewa kama mayai ndiyo maana wazazi wengi malezi yamewashinda na hawawezi kufanya chochote.

Akashauri kuwa ni muhimu kwa kila mzazi kutenga muda wa kuwalea watoto wake katika misingi ya maadili mema badala ya kuwaacha kujifunza tamaduni za kigeni ambazo baadhi yake hazikidhi misingi ya Kitanzania.

Amesema matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii yamekuwa yakichangia vijana kuingia katika makundi yasiyo na maadili, hali inayoweza kuhatarisha ustawi wa jamii na kupunguza uzalendo miongoni mwa vijana.

Amesisitiza kuwa malezi bora ya watoto ni msingi muhimu wa kulinda taifa huku akitoa mwito kwa jamii nzima kushiriki katika kuwaongoza vijana ili wawe na maadili mema na yenye manufaa kwa taifa.

Wakati huohuo, serikali imesema maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu, yatafanyika kwa kilele chake Juni 30 katika mikoa yote nchini.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni "Mtoto ni Malezi; Msingi wa Familia Bora kwa Taifa Imara," ikisisitiza kuwa familia ndiyo msingi wa kwanza wa malezi ya mtoto.

Kaulimbiu hiyo inahamasisha wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha watoto wanapata malezi chanya, upendo, ulinzi na usalama kuanzia kipindi cha ujauzito hadi wanapofikisha umri wa miaka 18 ili kujenga Taifa lenye wananchi wenye maadili na maendeleo endelevu.

# Marathoni


MAC D MARATHON 2026
MARATHON MAC D KUNDUCHI MARATHON
4TH JULY, 2026
NDC GROUND KUNDUCHI
Jisajili sasa
35,000Tsh.
www.macdmarathon.com
KWA MSAADA PIGA
0719 799 848 au 0702 562 009









# Wanaume mnaonyanyaswa fungukeni

HABARI za leo msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Wiki hii nitazungumza kuhusu ukatili wanaofanyiwa wanaume.

Imezoeleka katika jamii kuwa vitendo vingi vya ukatili hufanywa na wanaume dhidi ya wanawake.

Lakini upo ukweli ambao umejificha kuwa siku hizi kuna baadhi ya wanaume nao wanapitia changamoto ya kufanyiwa vitendo vya ukatili na wanawake.

Haya hutokea katika ndoa au uchumba. Tatizo ni wanaume kuwa kimya, kwamba mwanaume anaona aibu mbele ya jamii kueleza endapo anapigwa au kunyanywaswa na mwanamke.

Lakini kwa kufanya hivi wanaume hawa wanajinyima haki wao wenyewe kwani matatizo yao hayashughulikiwi ipasavyo na pia wanazidi kuiumiza jamii kwani vitendo hivi vinazidi kushamiri kimyakimya.

Wanaume wanapofumbia macho ukatili huo hupata madhara mbalimbali ikiwemo kuwaumiza watu watatu ambao ni mwenyewe, mkewe ambaye hajapata msaada wa kubadilika, na watoto wake ambao kupitia mambo anayopitia baba yao wanajifunza kuwa ndoa ni mateso.

Pia, kunyanyaswa kwa wanaume huonekana fedheha ikiwa jamii itajua, hivyo, kuweza hata kupata msongo na madhara yake ni makubwa zaidi.

Watoto wa kiume nao pia huathirika zaisi wanapobaini kuwa baba zao wananyanyasika ndani ya ndoa.

Kunyanyaswa kwa wanaume, huwajengea watoto wa kiume kuona kwamba 'mwanaume ni mfuko wa kupigwa' huku mtoto wa kike akijifunza ‘kupiga ndio lugha ya kupenda' na kuwafanya waibebe hali hiyo mioyoni mwao siku zote.

Mwanaume anayepitia changamoto hiyo anatakiwa kutokaa kimya, bali kupaza sauti na kueleza wazi kuhusu ukatili anaopitia.

Mwanamume anayepitia hali hii hapaswi kurejesha kwa kunyanyasa. Anatakiwa kukaa na mwenza wake na kumweleza kuwa anachokifanya si sahihi. Na wakati unasema haya usitumie hasira wala ukali.

Ili kukomesha pia hali hiyo unatakiwa kujilinda kisheria kwa kuripoti vitedo hivyo katika kituo chochote cha Polisi ili sheria ichukie mkondo wake.

Mwanaume hifadhi ushahidi kama vile picha za majeraha, meseji za matusi kwani vitakusaidia kupata haki yako kikamilifu.

Hata hivyo, kwenda mbele ya sheria iwe sehemu ya mwisho kabisa, kubwa yafaa iwe kufanya mazungumzo ya wawili na ikiwezekana hata kushirikisha wengine mnaowaamini kusuluhisha kadhia ya ugomvi.

Tukutane wiki ijayo

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Epuka kuvaa nguo zenye rangi nyingi kazini

KATIKA safu hii, leo tutaangalia mavazi ya kazini yatakayokufanya uonekane nadhifu.

Mambo muhimu ya kuzingatia;

*Jitahidi uwe na shati/blauzi ya rangi nyeupe au bluu bahari. Rangi hizo hukufanya uonekane nadhifu sana.

*Suruali ya rangi nyeusi, bluu bahari au iliyokolea na kijivu.

*Kwa upande wa sketi; hakikisha pia unayo ya rangi ya bluu bahari na nyeusi. Jitahidi upate zile nzuri unazoweza kuvalia shati au blauzi.

*Magauni; hapa cheza na mitindo kulingana na umbo la penseli, marinda zenye pemlamu ili zikusaidie pia kuficha kama una tumbo. Lakini pia ni muhimu kuzingatia rangi.

Watalaamu wa mavazi wanashauri kwa kazini jitahidi kuvaa nguo zenye rangi chache kama sio moja, kama unapendelea rangi nyingi basi kuwa makini na mpangilio wa hizo rangi au maua.

Jitahidi kuepuka kuvaa rangi zinazong'aa.



# Tumia 'scrub' hii kung'arisha ngozi

WATU wengi hawana utaratibu wa kutumia scrub zaidi ya kupaka tu mafuta. Lakini ukweli ni kwamba scrub zina umuhimu katika kung'arisha ngozi yako na kuwa na afya.

Leo nakuletea scrub yenye mchanganyiko wa sukari, kahawa, manjano na asali.

Mambo ya kuzingatia;

*Changanya kijiko kimoja cha sukari, kahawa kijiko kimoja, manjano kijiko kimoja na asali.

*Changanya mchanganyiko wako vizuri halafu ipake usoni iache kwa dakika tano kisha safisha uso wako vizuri.

*Kwa matokeo mazuri hakikisha unatumia kila siku kwa wiki mbili mfululizo







# Shakira katika penzi jipya

Na Mwandishi WETU

MWANAMUZI kutoka Colombia, Shakira Isabel amemtambulisha mpenzi wake mpya ambaye ni mwigizaji wa filamu, Lucien Laviscount.

Shakira ambaye ana umri wa miaka 49 anatofautiana umri na mpenzi wake huyo mpya kwa miaka 15.

Msanii huyo ambaye amepewa jukumu la kutengeneza wimbo rasmi wa fainali za Kombe la Dunia baada ya mafanikio ya wimbo wake wa Waka Waka (This Time for Afrika), amezua mjadala kutokana na uhusiano wake huo na kijana huyo mwenye umri wa miaka 34.

Laviscount anayejulikana kwa majukumu yake katika kipindi cha televisheni Waterloo Road na mfululizo maarufu wa Netflix Emily in Paris, alionekana akila chakula cha jioni na Shakira katika Jiji la New York na baadaye walionekana pamoja hadharani mara kadhaa.

# Romy afafanua ugomvi na mkewe

Na Mwandishi WETU

MWIGIZAJI wa filamu nchini, Romy Jons amejibu kauli ya mke wake, Kay Jons kuhusu madai ya kuachana.

Akifafanua kupitia ukurasa wake wa Instagram, Romy amesema ameoa mke wa pili na ndoa yake ni ya wake wawili jambo ambalo mke wa kwanza hakubaliani nalo.

"Nimeoa mke wa pili, mke mkubwa hataki kukubaliana nalo… bado ninawapenda wake zangu wote na siko tayari kumpoteza yeyote kati yao" amesema Romy Jons.

Aidha ameiomba familia yake kuingilia kati ili kusaidia kumaliza mgogoro huo kwa amani baada ya kuachana.





Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Deniz Undav akishangilia bao la pili alilolifunga dakika za jioni katika mchezo wao dhidi ya Ivory Coast juzi. Mchezo huo uliisha kwa matokeo ya 2-1. (Picha na Sportsnet)

# Hatua muhimu kutambua wababe yafika

JOTO la Trionda linazidi kushika kasi baada ya siku kumi na mbili za Fainali za Kombe la Dunia FIFA 2026. Tayali mafuta na maji vimeanza kujitenga kwa mataifa yanayokata tiketi ya kutinga 32 bora.


Wakati wenyeji-wenza Mexico na Marekani wakitinga hatua hiyo baada ya kushinda michezo yao miwili ya hatua ya makundi, mataifa mengine ambayo yamejihakikishia hatua hiyo ya mtoano ni Ujerumani kutoka kundi E, Uholanzi kutoka F.

Fainali hizo zilianza juni 11 mwaka huu kwa wenyeji wa mataifa matatu; Canada, Marekani na Mexico kuungana na mataifa 48. Hadi jana, mataifa matatu yameanga fainali hizo hata kabla "chakula hakijatengwa mezani."

Mataifa hayo ni Haiti kutoka kundi C, Uturuki kutoka kundi D, na Tunisia kutoka kundi F, hiyo ni kutokana na matokeo ambayo timu hizo zimeyapata kutokana na sheria ya kupata timu bora za mshindi wa tatu kutoka makundi 8 ambazo zimekuwa na matokeo bora kwenye msimamo wa nafsi hiyo kwa makundi yote 12.

Hata hivyo, Bara la Afrika ambalo linawakilishwa na mataifa 10, huenda mzunguko huu wa mashindano ya 23 yakashuhudia uwakilishi wa mataifa mengi kutinga hatua yakawa hafifu, licha ya kuwa bado safari ni ndefu ya kufikia hatua ya fainali ambayo itakuwa ni historia kwa Waafrika wote.





Kiungo Mkabaji wa Azam, Himid Mao Mkami akishangilia bao la kwanza alilolifunga wakati wa mchezo wao dhidi ya Yanga jana.

# Sasa ni Mzizima Derby Fainali CRDB

**Na John MARWA**

HATIMAYE ni Mzizima Derby Fainali ya Kombe la Shirikisho (CRDB Federation Cup) kati ya "Mnyama" Simba dhidi ya "Matajiri" Azam FC.

Azam FC imetinga hatua hiyo ya fainalia baada ya kuwaondoa mabingwa watetezi - Yanga hapo jana kwenye Uwanja wa Kirumba, Mwanza. Mchezo huo ulichezwa kwa dakika 120. Mabao yaliyofungwa - yote kwa njia ya vichwa yalikuwa ni 3-2.

Katika mchezo huo uliokuwa wa kusisimua, mtanange huo wa kusisimua Azam FC walipata mabao kupitia kwa Himid Mao Mkami, Lameck Lawi na Jephte Kitambala huku Yanga wakipata mabao yao kupitia kwa Bakari Mwamnyeto na Prince Dube.

Licha ya Azam FC kupata kadi nyekundu dakika ya 70 ya mchezo huo kwa Yoro Diaby, timu hiyo ilionyesha upinzani mkubwa wa haja.

Sasa ni rasmi Fainali ya CRDB Federation Cup ni Simba dhidi ya Azam FC. Mnyama Simba alitinga fainali kwa kuwaondosha Coastal Union kwa mabao 4-0.

Mshindi wa kombe hilo lazima atakuwa Simba au Azam, lakini mwenye kuamua ni kipyenga cha mwamuzi baada ya dakika 90, au 120 na pengine matuta ili kumpata bingwa mpya baada ya Yanga ambao wamekuwa mabingwa kwa misimu minne mtawalia kuondoshwa.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION